BE WITH YOU..2_5

Mtunzi Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 1 ($2)

Naysha baada kukutana na Nash basi alianza kulia sana tu maana kwake hamna kitu kilishawahi kwenda sawa kwenye maisha yale Nash akawa anambembeleza anyamaze

"Mimi hamna kitu kilishawahi kwenda sawa kwenye maisha yangu kaka Nash mwenzio nina ujauzito na kazi nimefukuzwa kazi baba yupo kitandani mgonjwa mimi nafanyaje kaka sielewi nitawezaje kulipa matibabu ya baba yangu nitaishije mimi"alikiwa anaongea Naysha huku akiwa nalia maskini maana muda huo hakujua afanye nini

" You no what Nay im here with you nothing gonna be  wrong i will fix every thing for you"aliongea Nash akimaanisha kuwa yuko na yeye na hakuna kitakacho enda vibaya kila kitu atakiweka sawa

" And if your tired enda tell him aku divorce"aliongezea Nash kuwa akiona amechoka aombe apewe taraka tu maana yeue hashindwi kumtunza

" Kaka naogopa sana ataacha kutoa hela kwaajili ya matibabu ya baba yangu acha tu nivumilie"alionge Naysha akakaa kidogo na kaka yake baada ya hapo akarudi zake nyumban alivofika basi aliingia ndani akalala tu akiwa ameshikilia tumbo lake

" Mwanangu mama yako nakupenda sna usije ukafikiria kitu chohcote kibaya mama atakulinda sawa mwanangu"alikuwa anaongea uku akiwa ameshikilia tumbo lake akalala tu hadi mchana alanyanyuka akaenda kupika chakula chake akala kidogo tu kingine akabeba akampelekea mlinzi akakaa naye kidogo wakawa wanapiga story kidogo

Jion Ikh alirudi akiwa mwenyewe sijui mwanamke wake alimuacha wapi baada ya kufika alimuita Naysha seblen baada ya kufika akamwambia

"Mama atapiga simu muda sio mrefu akikuuliza kuhusu suala la wewe kuacha kazi basi mwambie umechoka unataka kukaa nyumban hutaki kazi sasa ole wako useme tofauti ole wako"alionge Ikh akiwa anamuangalia Naysha kwa jicho kali kweli la msisitizo

" Sawa" yaani kwa kipindi icho Naysha jibu lake ilikuwa ni sawa tu ili kuepusha shari,dakika tano baadae simu iliit na aliyepiga alikuwa ni mama yake Ikh

" Mama niko apa na mkweo amekaa tu hana shida unaweza kuonge naye"alionge ivo Ikh baada ya simu kupokelewa

"Sawa mpe simu maana ni muda mrefu kweli sijaongsa naye" alionge mama yake Ikh

Akampa Naysha simu akaipokea
"Shikamoo mama"alisalimia Naysha kwa utulivu kabisa na heshima na hicho ndo mama mkwe wake anapenda
" Marhaba mwanangu unaendeleaje maana hatujawasiliana tuna muda mrefu"alionge mama Ikh
" Niko salama mama nimekukumbuka sana"aliongea Naysha lwa uchangamfu
" Nimekukumbuka pia,em niambie kwanini umeamua kuacha kazi mwanangu?"aliuliza mama Ikh maana hakupenda mkwewe kuach Kazi

"Mama nimeona mume wangu akitoka kazini anapata tabu sana na mimi nakuwa nimechoka sana nashindwa kumhudimia mume wangu vizuri" aliongea Naysha na kutoa maelezo ambayo yalimuingia mama Ikh na kuona kuw ana mkwe anayejali kuhusu mwanae alijisikia faraja sana

" Sawa mwanangu basi mwambie Ikh atafute siku mje kunitembelea sawa mwanangu" Naysha aliitikia sawa mama na simu ikakatwa na Naysha akanyanyuka akaenda nje chumbani kwake bila hat kumuongelssha Ikh ile hali ya kutoka kimya kimya ilimkera Ikh kwanini ametoka bila kumuongelesha alitamani hata atoke akamchokoze lakini akaona haina maana akaingia tu chumbani kwake, usiku sana akiwa anachati whatsapp iliingia meseji

"Angalia izo picha kila mara nakwambia huyo demu hajatulia we muda wote unamng'ang'ania angalia sasa kakuaga yuko safari wakati yuko apa apa Iringa" alikuwa ni rafiki yake Fatih na alimtumia picha za Naiphat akiwa na mwanaume mwingine tena akiwa kajiachia kabisa,yaani Ikh alianza kutetemeka maana hakuwahi mfikiria Naiphat kama anaweza fanya ujinga wa aina hiyo na alimuamini sana yaani ile sana tu

" Uko sehemu gani nataka kuja sasa hivi"

Fatih alimuelekeza sehemu yenyewe na baada ya kufika pale kweli alimshuhudia Naiphat akiwa na mwanaume mwingne akiwa anabishana naye sana Ikh akaona aangalie kinachoendelea lakini alikuwa na hasira sana.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 02 ($2)
Tulipoishia ..........

Baada ya Ikh kwenda na kumfuma Naiphat kumbe bhana Naiphat alimuona wakati anaingia hivyo akamtonya yule mwanaume ajifanye kuwa ndo anamtongoza wakati ilikuwa ni kweli mwanaumr wake akawa anaifanya mkali hadi anamsukuma yule kaka Ikh baada ya kuona kama Naiphat anaitetea aliwasogelea pale akakuta Naiphat anamwambia Uyo mkaka kuwa yeye amtaki

" Nilishakwambia mimi sikutaki na usinifate fate mimi nina mwanaume wangu na nampenda sana tu wewe sio muelwwa hata kidogo"aliongea Naiphat kw sauti sana yaani alifanya makusudi ili kuuvutia umati wa watu walokuwepo kwenye klabu ile waangalie nini kiachoendslea basi ni kweli watu waliacha kunywa wakageuka kuangalia nini kinaendelea

" Mimi siwezi kukubali kwani ni kitu gani anachokupa uyo mwanaume ambacho mimi nitashindwa kukup mbona na mimi nina pes na mwanaume mzuri tu nikubalie basi"aliongea yule kijana lakin kabla hata hajamaliza kuongea alikula ngumi ya mdomo na ni kama hakutarajia alipivwa Ikh na akamvuta Naiphat nyum ya mgongo wake ili apambane na uyo mwanaume mwenzake alimpiga yule kaka mpaka akawa hawezi kunyanyuka watu wakawa wanamuomba amwache baada ya kulidhika

" Uwe na heshima na wanawake wa watu kijana" aliongea hivyo Ikh yulr kijana alifuta damu kwenye pembe ya mdomo wame akacheka kwa dharau akiwa bado yuko pale pale chini Ikh hakujali sana hicho kitu alichokifanya yeye alimnyanyua  Naiphat akaondoka mazingira yale akiwa ana hasira sana sasa muda huo Naiphat alikuwa anatafuta namna ya kumbembeleza na akakosa kabisa hakujua nini,maana kwanza alimdanganya amesafiri yuko nje ya Iringa lakini kafumwa akiwa yuko ha hapo tena na mwanaume mwingine,Walivofika nyumban Ikh alishuka wala hata hakutaka kumsubiri Naiphat akaongiza njia hadi ndani Naiphat ikabidi amkimbilie

" Babe haiko kama hivyo mimi sikukudanganya nilitaka niondoke kesho leo ndo nikatoka niende kutembe kidogo ndo nikakutana na hayo majanga me yule kaka simjui"aliongea Naiphat akiwa amepiga magoti maana alijua tayari ashalivuruga

" Mara ya mwisho nilikwambiaje kuhusu mambo ya club?" alimuuliza Naiphat akiwa kamkazia jicho

" Ulinambia nisiende club babe"alijibu Naiphat kwa kujiuma uma maana alishakatazwa kwenda club

" Sasa wewe pale ulifata nini wakati unajua kabisa nilishazuia usiende kama maeneo hayo"aliongea vie kwa hasira kweli

" Babe nisikilize nikwambie kwanza" alitaka kujitetea lakin Ikh hakumpa nafasi maana alikuwz na hasira kweli yaani hamna kitu hapendi kama kuongea au kukukataza kitu alafu urudie kukifanya hapendi alianza kutoka nje maana hakutaka story nyingi na Naiphat akataka kumfata akamwambia

" Bora hata usinifate maana nitakupiga nikuumize bure rudi ndani ukalale niache mwenyewe" aliovoongea hivo alitoka nje akaenda kumgongea Naiysha mlango na kuda huo ilikiwa saa sita usik alifungua mlango akamwambia

" Nakusikiliza mbona usiku usiku"aliuliza Naysha kwa sauti ya usingizi kweli yaani alikuwa anasinzia

" Nipishe naomba kulala uko ndani" aliongea Ikh akiomba kupishwa mlangon Naysha hakutaka kuhoji alimruhusu akaingia na yeye akaingia akatoa mashuka mengine ksenye kabati akataka kutandika chini na muda huo Ikh alikuwa anamuangalia alivoona anataka kutandika akamshika mkono kumzuia

" Acha tu naomb nikuombe kitu panda kitandani nataka nikukumbatie sikufanyi chochote nakuomba" alionge kwa upole tofauti n siku zote Naysha so mwanamke wa kubishana sana alitaka tu kutimiza wajibu wake kama mke na kipindi hicho ujaizito wake mara nyingi ulitaka sana kuwa karibu na Ikh hivyo hakutaka kabisa kuipoteza nafasi hiyo aliweka yale mashuka apanda kitandani Ikh akamkumbatia taratibu kabisa akapeleka mkono kwenye bedside akazima ile taa pakawa giza akamwambia Naysha asihofu hawezi kumfanyia kitu chochote kibaya na ni kweli yaani mpaka kunakucha asubuhi hakuwa amemfanya kitu chohcote kabisa na mtu wa kwanza kuamka

Alikuwa ni Naysha aliamka akakuta kalala kifuani Ikh na mkono mmoja wa Ikh ulipita maeneo ya kiunoni na mwingine alikuwa amekuwekea kichwan kuonyesha kwamba usiku wakati yeye akiwa amelala Ikh alikuwa anapapapasa nywele zake mpaka akaja kupitiwa na usingizi,Naysha alitumia muda kidogo kumtazama mwanaume huo mwenye sura nzuri na anaonekana kama Malaika akiwa kalala lakin akiamka ana mdomo mchafu kuliko kawaida mkono mwepesi yaani hachelewi kukushushia kofi basi alivyochoka kumtazama alijitoa taratibu akamfunika blanket vizuri akatoka nje kuendelea na majukumu mengine anayoyafanyaga kila siku lakini mara kwa mara alikuwa anasikia

kizunguzungu ila alijikaza tu na siku hiyo alimuomba mlinzi amsaidie kumwagilia bustani maana hakuwa anajisikia vizuri hata kidogo na mlinzi kwasababu aliidhi naye vizuri alikubali akamsaidia na kazi zingine alizoweza alimwambia kama anashindwa kupika basi aache atapila yeye lakini Naysha alikataa akamwambia labda wasaidiane,hivo waliongozana jikoni  wakawa wanapika pamoja yeye na mlinzi

Saa moja kasoro ndo muda ambao Ikh aliamka akajikuta kitandani peke yake akajikuta tu bila kutajarajia ametabasamu mwenyewe maana Naysha ni binti hivi amejaliwa kila kitu mpole ana sura nzuri ana adabu yaani tabia nzuri zote alikuwa nazo yeye lakini aiju tu kwanini hakumpenda akampenda yule mapepe ,basi alijinyanyua taratibu kabisa akaenda ndani sasa alisikia watu wanacheka jikoni si ndo ikabidi asogee akakuta Naysha kakaa kwenye kiti alafu mlinzi yuko anamsaidia kupika sasa alikuwa naruka huyo mafuta yakipiga kelele kidogo basi yeye anatamani kupaa sasa Naysha icho ndo kilichomiwa kinamchekesha Naysha,Ikh alivosogea

mlangoni na kumuona Naysha akiwa na tabasamu basi sijui ilikuwa vipi lakini naye alijikuta anatabasam akawaacha waendelee  kuenjoy akaingia ndani akaoga kwanza alafu akaenda kuvaa mavazi yakw ya kazi ambayo tayari Naysha alishamuandalia akaatoka selblen naye Naiphat ndo huo muda alitoka ndani akajaribu kujibebisha lakini alikuta mtu kaweka sur ya kazi hataki ata story ikabidi akae tu kimya,walivomaliza wakwenda kazini walienda na walubaki walibaki

ikapta kama week hivi Ikh halali ndani alikuwa bado ana hasira na Naiphat kwa kwenda club hivo aliona bora aendelee kulala tu kwa Naysha na muda ambao alikuwa nalala kwaNaysha alikuwa anajisikia amani sna na kuna muda basi alitamani hata angekuwa wanaishi hivo siku zote.

Sasa siku hiyo baada ya Naiphat kuona mambo yanazidi kuw mabaya Iwake aliona amtafute dada ake Naysha ambaye ni Naishia akampigia sim

" Hellow"ilisikia sauti ya Naishia baada ya simu kupokelew

" Mambo mpenzi"aliongea Naiphat

" Pw za kupotea mpaka tunaanza kukutafuta kama mshale wa saa nini dada?" aliongea kwa utani Naishia

" We acha tu mwenzio sina amani ni week sasa toka nimelikoroga kwa Ikh hataki hata kuniona yaani hataki kabisa sijui nifanyaje saivi ndo anajifanya yuko busy na mkewe" alionge Naiphat

" Pole we naye uache kuzubaa mwanaume wa kwako alafu unashindwa kumtuliza unamuacha uyo mjinga ammiliki em jiongeze bas"

" Nitaiongezaje Naishia wakati toka alivooa na nilivorudi yaani tunalala kitanda kimoja lakini hakuna cha maan anachokifanyaa ni kama ananinyali hivi yaani ataishia tu kukubusu alafu ukijaribu kumushawishi msex anakukwepa sijui shida nini" aliongea Naiphat kimbe sasa shoga anavumilia muda wote kujifanya anapendwa kupmbe ndani mambo mabaya
" Me nitakupa njia" aliongea hivo Naishia.

Je ni njia gani?
Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 03 ($2)
Tulipoishia.....
Naiphat baada ya kuona mambo yanamuendea kombo aliamua kumtafuta Naishia dada wa Naysha akamwambia kuwa mambo yanamiendea kombo
" Usijali mbona hilo ni jambo dogo tu unawaza kwanza mbona kuna njia kibao za lusuluhisha hilo"alionge Naishia
" Njia gani naweza kuzitumia maana kama kumbembeleza nimebembeleza adi nimechoka saiv adi analala na Naysha na sijui usiku huwa wanafanya nini yaani kichwa kinaniuma kwakweli" Alilalamika Naiphat
" Usijal kwani uko danger kwanza?" aliuliza Naishia

" Yeah niko danger vipi kwani"aliuliza Naiphat maana hakuelewa alikuwa na maana gani kumuuliza ivo

" Unatakiwa kubeba mimba haraka sana ukibeba mimba lazima atataka kubaki na wewe hivyo taraka lazima atoe na utatumia chance hiyo ili amuache uyo mtoto wa kahaba"

" Lakin mimba me apana me bado siko tayari kuzaa jaman sitaki kuharibu shepu yangu"aliongea Naphat

" Aya endelea kuwaza shepu alafu mwanaume analuacha apo ndo utakoma na kwa shelu gani unayoiwazia kwanza?"Naiphat ata hakumkopesha alimpa maana ni kweli shepu hana

" Mmmh basi yaishe niambie sasa nafanyaje mpaka nilale naye"aliuliza Naiphat akiwa mpole maana aliambiwa ukweli

" Kuna dawa nitakutumia utamchanganyia kwenye kinywaji lazima atataka mwanamke wa kulala naye tu hivyo we tulia"

" Basi sawa niambie uko wapi niifate" naiphat hakutaka kusubiri alinyanyuka muda huo huo ambao aliambiwa na kuelekezw sehemu alipo alikod tax safari ukawa ni kwenda huko sasa.

Ilipofika jioni basi Naysha kwasababu yeye alikuwa hana kazi yoyote anashinda nyumbani tu na akitoka hapo hivo nyumban basi angeenda kumuona baba yake au kukutana na kaka yake wa hiari tofauti na hapo alikuwa nyumbani tu akihangaika kulea mimba yake maana ilikuwa inamsumbua kweli na hakuwa amemwambia mtu mwingne yoyotw tofauti na Nash kaka ake na Swalha toka alivohama nchi basi kupatikana kwake ikawa ni tabu sana hivyo aliamua tu kukaa nalo moyoni.Sasa siku hiyo jion akiwa jikoni anaandaa chakula akashangaa kwa mara ya kwanza toka ameingia kwenye hiyo nyumb Naiphat anaingia jikoni maana alikuwaga anakataa na kusema

yeye hakuja hapo kuja kuwa mfanyakazi,alivoingia jikoni Naysha ata hakujishughulisha naye ye aliendelea tu na kazi zake naye Naiphat akawa anatengeneza kahawa ety kwaajili ya Ikhram ambaye alikuwa na kazi kwa muda huo alikuwa maktaba.Naysha aliona mahaba ya watu ye hafai kuyaingilia alivomaliza akatoka sasa alivotoka Naiphat baada ya kukamilisha kuandaa kahawa akatoa dawa flani akaweka kwenye ile kawaha alafu akabeba kumpelekea ikhram.

Alipofika akaweka sura ya huzuni Iwanza alikuwa amevaa ki nightdress cha mitego mitego tu maana alijua kwa vyovyote vile Iwo lazima lengo lake litimie alimpomkaribia Ikh akaanza kujiongelesha

" Najua nimekukosea sana kwa kutokukusikiliz Wewe na najuta sana kwa kitu nilichokifanya,hata kama una hasira na mimi usikasilikie adi chakula na vinywaji nimekuletea kahawa hii hapa upunguze usingizi najua uko busy sana"alikngea kwa ustaarabu hadi Ikh akamuonea huruma akamwambia ampe na Ikh alivochukua ile kahawa ainywa yote kwa wakati mmoja kwasababu alikuwa ana mambo mengi ya kufanya,hazikupita hata dakika kumi akaanza kujisikia joto ambalo si la kawaida alianza kufungua vifungo vya shati lake kimoja baada ya kingine mwisho wa siku alijikuta yuko kifua wazi kabisa lakini joto alikupungua yaani alikuwa anajiskia vibaya mno,muda

wote Naiphat alikuwa kasimama pembeni sasa baada ya kuona vile akajua tayari dawa imeanza kufanya kazi akamsogelea Ikh

" babe una shida gani ety mbona uko kama hivo" aliongea akiwa amemkumbatia Ikh kwa nyuma Ikh alimtoa mikono yake kwa nguvu maana apo akili yake ilikuwa inampeleka less vibaya sana

" Basi nikusaidie uende chumbani babe ukapumzike" Naiphat aliongea ivo akataka kumnyanyua kwenye kiti lakin alisukumizwa akajigonga uko kwenye kiti Ikh akaamka akiwa spidi ile mbaya atoka hadi nje,sasa muda huo Naysha ndo alikuwa ametoka kuoga yuko tu na kitaulo kifupi sana amesimama kwenye dressing table yake anafuta nywele maji akashangaa mtu kaingia kwa speed na alipofika yaani hakuuliza nini wala nini alifunga mlango na ufungua akautupia chini ya uvungu wa kitanda,baada ya kutupa ufunguo alimvamia Naysha na kuanza kumpa romance kwa nguvu na ni kitu ambacho hata yeye wenyewe Naysha hakukitegemea.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 04 ($2)

Tulipoishia.......

Naysha alishtukia akiwa amevamiwa na kupewa romance ya k8babe tena yaani kwa nguvu hutaki utafanya,unataka utafanya,Naysha ilibidi sasa aanze kujitetea maana hakutaka fujo kabisa japo kwenye uhalisia kwa kipindi hicho Naysha alishaanza kumpenda kiukweli ukweli Ikhram lakin kama ni hayo mambo basi walihitaji utulivu na sio kama hiyo staili alokuja nayo Ikh ukiangalia ye ana mimba ya miezi miwili sasa na hizo fujo alijua kabisa sio salama kwa mwanae hivyo akawa anajitahdo kujitoka kwa Ikh lakin hakuweza kabisa maana Ikh alimng'ang'ania kwa nguvu zote mwisho kabisa alivuta kitaulo cha Naysha akabaki akiwa mtupu kabisa Naysha kila

akijaribu kumponyoka aludakwa kwa kurudishwa kwenye himaya ya mwanaume,kwa mara pili tena Ikh alilala na Naysha kwa kumlazimisha bila kujali anaumia au haumii,sasa kumbe wakati wote Naiphat alikuja na kugonga sana kujaribu kumtoa Ikh mle ndani hakuna aliyemsikia kwa zile vurugu zake mpaka Ikh anaanza kufanya yake Naiphat alikuwa nje anasikiliza kila kitu akawa anamsikia tu Ikh alivokuwa anaugulia uko ndani utasema mtoto mdogo wakati akiwaga na yeye hajawahi kifanya hivo hata siku moja alijisikia wivu akataman ata akabomoe mlango aingie ndani akajitege yeye na kitu kilichomchanganya zaidi kwanini Ikh alimkimbia yeye akaja Kulala na Naysha

na wakati alishasema kabisa kuwa huyo ni mkewe wa mchongo na kwenye mashart yao basi hawaruhusiwi kusex, sasa kwanini kwenye hali kama hiyo alimkimbilia Naysha,yaani alijikuta yuko chumbani hakujua ata alifika fikaje maana alikuwa na mawazo debe na alijilaumua sana kw ujinga  dawa katafuta yeye alafu mambo kafaidi mwenzake yaani alilala akiwa na dukuduku moyoni mwake,wivu ulimsumbua sana.

Kulipokucha asubuhi Ikh aliamka taratibu bila kumsemesha Naysha ambaye alikuwa bado kalala huku macho yale yamevimba maan amelia usiku kucha na Ikh kwasababu alichanganyiwa na dawa yaani amekesha kifuani kwa Naysha bila huruma na wala kujali kama anaumia au laa hivyo Naysha alilia mpaka akachoka.

Sasa Ikh alivoamka alishazoea anakuta nguo tayari zimeshaandaliwa chai iko tayari siku hiyo paikuwa patupu hakuna cha chai hakuna kuandaliwa nguo maana Naysha ndo huyo alikuwa kalala hadi muda huo hakuamka sijui ni uchovu au ni nini haikujulikana.Baai ilibidi ajipasie nguo zake mwenyewe na hasira zake zote zilikuwa kwa huyo mpumbavu mmoja ambaye hakuona hata haya kumtilia dawa ili alale naye hivyo hakitala hata kumuamsha aliniandaa tu mwenyewe akapanda gari akaenda kazini.

Masaa yalisogea mpaka inafika saa nne mlango wa Naysha haukuwa umefunguliwa kabisa hadi mlinzi alipat wasiwasi,sasa kumbe kule ndani kutokana na zile hekaheka za usiku kucha na kukunjw Naysha tumbo lilianza kumuuma na kwa vile alikuwa ametandika mashuka meupe basi michilizi ya damu ilianza kuonekana alilia maskini na hakuwa tayari kumpoteza mwanae alijitahidi akaisogelea simu yake akatafuta namba ya Nash uzuri aliiipata na alikuwa na salio alimpigia akamuomba msaada aje kumbeba ampeleke hospital. Kweli hakuchukua muda Nash alifika pale na rafiki zake wawili  mmoja wa kike wakiafrika na yule mwanaume mwingine

alikuwa mzungu kama Nash walipofika walipiga honi mlinzi akafungua mlango akamwambia ameluja kumuona Naysha amuelekeze chumba chale kilipo kweli mlinzi akawaelkeza wakaenda wakavunja mlango maana ulikuw umefungwa kwa ndani baada ya kuingia Nash alihisi kuchanganyikiwa baada ya kumuangalia dada yale huyo wa hiari akiwa amelala kazima kabisa alafu kuna michilizi ya damu hakiweza kuvumilia alijikuta akidondosha machozi maana alijua kabisa huenda mimba inataka kutoka,yeye na rafiki yake walitoka nje yule binti ambaye walikuja naye akamnyanyu naysha akamchukulia kijora akamvalisha,ndipo nash aliingia walambeba hadi kwenye gari

wakaondoka.

Walipofika hospital Nash aliwaomba madokta wamsaidie kwa gharama yoyote ye yuko tayari kulipa na wafanywe wawezavyo mimba yake isitoke maana akija kugundua kuw mimba yake imetok basi atajilaumu maisha yake yote,basi Naysba alianza kupatiwa matibabu baada ya muda alirejewa na fahamu lakini alikiwa na dreap ya dam na maji akaambiwa asubiri zikishaisha atarudi nyumbani.zile dreap zilipoisha basi alitakiwa kuonana na docta kwanza kabla hajaondoka maana docta alisema kuna vitu vya kumwambia

" Naysha umeolewa?"aliuliza yule docta baada ya kukaa na Naysha akashindwa ajibu nini  maana mume mwenyewe wa mchongo na hajuo hata kama mkewe ana mimba,ikabidi Nash amsaidie kujibu
" yeah she is my wife" Nash alijibu ili kurahisisha mambo maana hawakutaka kupotez Muda ulikuwa umeenda sana saa nne kasoro usiku.
" Sasa Naysha cha kwanza nikushauri wewe na muomeo mr Nash,unafaa kuwa na muda mrefu sana wa kupumzika,pia unafaa kula vyakula vyenye vitamin kwa sana mana afya yako kidogo sio nzuri" aliongea yule docta na kuweka nukta kwanza
" Ndiyo docta nimekueleqa nitajitahid"alijibu Naysha

" kubwa zaidi na muhimu sana la kuzingatia sana sana,mimba yako inatishia kutoka yaani usipokuwa makini huyo mtoto utampotez Muda wowote ambao hata haujatarajia"dokta alivosema hivo alimfanya Naysha kushtuka sana maana katika vitu hataki kusikia basi nikumambiwa mara sijui mimba yake inataka kutoka aiseee hataki kabisa

"Sasa dokta nitafanyaje ili nimlinde mwanangu"aliongea Naysha akiw tayari kapanik Nash alichokifanya ni kumtuliza tu na kumwambia masikilize docta kwanza

" Kitu cha kwanza jitahidi sana kupunguza mawazo,cha pili uwe unapata muda mzuri wa kupumzika ,cha tatu usifanye kazi nzito ya aina yoyote na cha mwisho kabisa tena muhimu wewe mimba yako haitaki kabisa sex hivyo mumeo anafaa kukuvumilia kwa hichi kipindi yaani hamtakiwi kusex kabisa na siku utakayojichangnya ukasex basi ndo uhesabie mtoto umempoteza nafikiri hadi hapo umeshanielewa" yaani docta mpaka anamaliza kuongea Naysha mwili sio wake kabisa maana ni kama alishikwa nz bumbuwazi yaani katika hayo mashart yote aloona lina uwezekano kidogo la kupumzika na kupunguza mawazo lakini haya mawili jaman kwale

ulikwa ni mtihani atakaaje bila kufanya kazi wakati yeye kama mfanyakazi na vipi atamkwepa Ikhram mwanaume mwenye nguvu na asiye jali maana anaweza kulala naye kwa nguvu muda wowote vipi kuhusu mtoto wake? aisee kichwa kilimuuma yaani mpaka anafika kwenye gari hajui alifikaje kuwa alibebwa alitembea au alipaa yaani hajui kabisa Nash na marafiki zake walijisikia vibaya sana na walijua yupo kwenye kipindi kigumu sana. walimbeba kwenye gari na walipokaribia kwenye nyumba nanayoishi aliwaambia wamshushe maana wakifika tu wamatamponza na kufanya apigwe,walimuulza kama atakuwacsawa kwensa mwenyeqe akajibu ndiyo lakini wakaona sio vizuri

Nash akashuka akamsindikiza hadi karibu na getini akasimama kwa mbali akawa anaaangalia anavoenda.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 05 ($2)

tulipoishia....

Mida ya Jion baada ya Ikh na naiphat kurudi nyumbani kila mtu kivyake basi Ikh alitegemea atakuta ameandaliwa nguo za kubadilisha na chakula kingekuwepo lakini katika hivyo vyote vilwili hakuna hata kimoja ambacho kilifanyia akajiuliza kuna shida gani hadi inakuwa kama hivo aliamua kutoka nje na kumuulza mlinzi amwambie ni wapi Naysha alipo mpaka muda huo ikiwezekana amfate huk alipo akampige makpfi

" Habari yako Moze"alisalimia Ikh

" Salama tu boss karibu" apijibu Moze ambaye ndo mlinzi

" Asante ivi unaweza niambia Naysha yuko wapi mpaka saa hii saa mbili kasoro?"aliongea Ikh akiwa anaangalia saa yake ya mknoni, kwanza mlinzi alishtuka ikabidi amuulize

"Haaaaaa lwani boss hujui chochote?" aliuliza moze na kumfanya Ikh achanganyikiweaaana lwa akili yake ya haraka akajua tu Naysha katoroka

" Sijui nini em moze sem usinichanganye" ikh aliongea kwa ukali

" ujue boss itabidi tu nikushangae yaani mkeo kabebwa hapa hajitambui kazimia alafu wewe hujui?" yaani sauti ya Moze ilisikika kama mwangwi kwenye maskio ya Ikhram maan ilikuwa kama mzaha ety kazimia kwasbabu gani yaani kwa kipi?.

" Unasemaje moze ujue uache masihara yako mimi nikiwa nakuuliza vitu vya maana" Ikh alihisi labda Moze alikuwa akimtania maan mara nyingi sana anapenda utani

" Boss sidhani kama naweza leta utani kwenye suala la uhai na afya ya mtu ni kweli mida ya mchana walikuja wazungu wawili na mwanamke wa kiafrika mmoja wakambeba mkeo akiw kazimia kabisa na alikuwa na hali mbaya kwa kumuangalia tu wakaondoka naye na ndo hjarudi mpaka saivi ila walisema wanampeleka hospitali" Moze ilibidi aeleze yale anayoyajua basi baada ya kumwambia hivyo Ikh alijihisi hatia kidogo maana yeye asubuhi aliamka bila hata kumuuliza mtu umeamkaje akaondoka zake na wala hakumpigia sim kuilizia hali wakati alikuwa anajua kabisa  alichokifanya jana yake usiku, baada ya kupewa tarifa ile alikuwa haelewi afanye nini alijikta anaenda

mbele anarudi nyuma anawasha gari anaona kama haifani azima haelewi aanzie wapi kumtafuta Naysha maana hata hajui Naysha alipo Na kilichomuuma zaidi baada ya kuambiwa ni wazungu mdo walikuja akajua moja kwa moja ni yule mpenzi wa Naysha kama anavyoamini yeye sasa sijui kwanini yaani alijikuta anaumia kweli. Wakati akijwa hajui afanye nini mara alisikia kengele ya getini alitoka spidi hadi akamzidi mlinzi alipofungua alikutana na Naysha akiwa amechoka uso hauna nuru kabisa kuonyesha kuwa hayuko sawa,kwa wasiwasi alokuwa nao Ikh alijikuta amemkumbatia kwa nguvu na kuanza kuuliza maswali yasiyoeleweka

" Uko salama? kwanini hukuniambia kama unaumwa? unasahau kama mimi ni mume wako? uko sawa sasa unasumbuliwa na nini em niambie wapi panauma" yaani kw mara yackwanza Ikh alikuwa na wasiwasi na Naysha kuliko kawaida hadi mlinzi alishangaa maan hajawai kuona Ikh akiwa na wasiwasi namna ile hata alipoambiwa Naiphat anaumwa sijui yuko hoi hakuwahi kuwa hivyo basi mlizni akaona apunguze umbea akakaa kimya

"Niko sawa" Naysha kabla hata hajajibu basi alijisikia kizunguzung alataka kudondoka na Ikh akawahi kumdaka akambemba akampeleka hadi chumbani kwake kwa mara pili toka Naysha ahamie kwenyw hiy nyumba alipofika alikuta Naiphat amelala kihasara hasara akamwambia

" Nyanyuka nenda chumba cha wageni nahitaji kumtunza Naysha hayko sawa" yaani aliongea maelezo machache lakini yaliyoshiba maanake hakutaka mtu mwingine mule ndani alitaka kubaki na mkewe wawili

" Lakin babe...." Kabla hata Naiphat hajamaliza kuongea alikatishwa

" Hakuna cha lakini nyanyuka utoke bhana nadhani unanijua toka apa kwanza bado nina hasira na wewe"baada ya Ikh kusema hivyo Naiphat alijijizoa zoa akatoka mpaka nje lakin alibamiza mlango kwa nguvu mpama iki akataka lunyanyuka akampe funzo maana hamna kit anachukia kama dharau lakin wakati alivyotaka kunyanyuka alishikwa mkono na Naysha akiwa anatetemeka sana Alafu kafumba macho

" Usiniache naogopa sana,usiniache" hayo yalikuwa ni maneno ya Naysha ambaye aliongea akiwa maefumba macho Ikh akarudi taratibu akakaa

" Sawa mama me sitoka ata niko apa na wewe usiogope sawa?" aliongea Ikh na sijui ayo maneno aliyatoa wapi maana yeye na Naysha hazijawahi waka hata siku moja, basi alimfunika Naysja shuka vizur akapanda naye kitandani akamkumbatia taratibu kabisa ili kumuongezea joto maana alihisi labda lile joto la blanket alitoshi akawa ananusa alufu ya mkewe huyo wa mchongo taratibu alikuwa na karufu flani hivi unique sana ambacho toka Ikh anakua alishawahi lukisikia kwa mtu mmoj tu ambaye alilala naye kwenye ile hotel mara ya mwisho na hakumjua

" Nisamehe naahidi sitarudia kifanya huu ujinga wangu naamini hutonikasirikia" aliongea Ikh aliwa anambembsleza Naysha aliyekuwa na usingizi wenye maumivu kwa ndani,sasa kuna muda sijui aliota ndoto mbaya akamshika Ikh lwa nguvu akamwambia

" Nisaidie me sitaki kupigwa kaka Nash" aliongea hivyo na kitaja jina la mwanaume aliyemuita kaka Ikh ikabidi afikirie kwanza maana toka yeye amemfahamu Naysha anajua kabisa Naysha ana dada tu ila kaka hana na akahisi kabisa ilo jina alishawahi lisikia sehemu ndo kuvuta kumbukumbu akakumbuka ni yule mzungu,apo ndo alipoanza kujialumu maana alihisi labda Naysha anadate na yule mzungu kumbe anamheshim kama kaka yake,alichokifanya basi alimkumbatia Naysja tu kwa nguvu ili asiendelee kuota ndoto mbaya na alijua ni yeye ndo anayemuota maana ndo huwa anampiga.

Upande wa pili sasa baada ya Naiphat kutoka pale chumbani alikuwa na hasira sana alichokifanya alimpigia sim Naishia ilipopokelwwa

" Naona kabisa naenda kifa ivi ujaua kama huyu mwanamke humu ndani anajifanya mgonjwa yaani anavojidekeza" aliongea Naiphat kwa hasira

" Heeee we naye yaani uyo mtoto mdogo ndo amekushinda kama vipi sema nije kukusaidia?" aliongea Naishia maana yeye mwenyewe alikuwa anamtamani Ikhram maan mumewe mwenyeww yuko busy hataki hata kuwa na muda naye

" We tulia nishampangia mpango mzuri tu nitamnyoosha asifikiri kuwa yeye ndo ana akili sana" aliongea Naiphat na kukata simu.

Ni mpango gani huo alio nao Naipht? Tukutane sehemu ijayo.BE WITH YOU.2.6_10

Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 06 ($2)
Tulipoishia.......
Usiku kucha Naiphat alikuw akipanga namna ya kumkomesha Naysha na kusababisha hadi apewe taraka maana yeye alitaka kuolewa sasa

" Unasema nini wewe maye usolalaga usiku kazi kusumbua watu" aliongea kwa ukali naada ya kupokea simu

"Naiphat nimekumisi mke wangu unajua toka umeniacha siku ile bar hatujaonana tena me nataka uje unione basi ata siku moja"aliongea mwanaume wa upande wa pili na hiyo ilidhirisha kiwa ni yule mwanaume wa usiku bar

" Em koma wewe kwanza kuanzia sasa nataka niachane na wewe niolewe nimechoka na mauongo yako,kipindi kile ulinidanganya unanioa nikamuacha Ikh kwasababu yako alafu uakishia tu kunitumia ulivochoka ukanambia hunitaki kwa muda huo nirudi kwa Ikh,unafikiri nataka kurudia tena kosa? kama Ikh alinikubali mara hii nikirudia itakuwa ndo basi tena hivyo sitaki kurudia kosa kabisa kwaheri na ukome kunitafuta" aliongea hivyo Naiphat akakata simu akiwa na hasira sana meseji iliingia kwenye simu yake ikisomeka hivi

" Mimi siachwagi kirahis na sijawahi achwa huwa naacha sasa subir uone kitakachotokea" meseji hiyo ilitoka kwa yule mwanae tusiyemfahamu jina
" Shit rock kwenye hili huwezi nizuia ikibid nitakupotez kwenye uso wa dunia siwezi kukubali unavurugie malengo yangu" Naiphat aliongea mwenywe kwa hasira sana akazima simu akalala

Ilipofika asubuhi Ikh alikuwa wa kwanza kuamka aliamka taratibu akamfunika vizuri Naysha akatoka hadi sebleni akaangalia kwenye friji kitu chochote cha kupika akachukua ndizi na nyama akaenda kumuandalia mchemsho mgonjwa na soseji mbili akazitumbukiza kwenye tambi.

wakati akiwa anaandaa alikuwa Naiphat akamkumbatia Ikh kwa nyuma lakin Ikh wala hakuonyesha kuchangamka kama siku zote alimtoa tu mikono

" Babe unaniandalia kifungua kinywa"aliongea Naiphat kiwa anamrembulia Ikh ambaye hakuwa na muda naye

" Nafikiri wewe pia una mikono unaweza tu andaa chai yako hii ni kwaajili ya mgonjwa" Aliongea Ikh na kumfanya Naiphat ajisikie aibu na hasira kwa ndani,yaani yeye toka ameanza mahusiano na Ikh wana mwanka na miezi kadhaa lakini hajawahi hata kumchemshia chai tu ile ya kuweka majani ya chai leo na sukari na maji ila leo yuko jikoni busy kabisa anamuandalia break fast ya nguvu Naysha ambaye wamejuana miezi minne tu iliyopita roho ilimuuma sana katok taratibu kule jikoni akajianda akatoka bila kuaga.

Dakika ishirini baadae kifungua kinywa kilikiwa tayari akabeba akaingia nacjo cumbani kwake akamwamsha Naysha alikuwa anajvuta sana kuamka akamsaidia kpeleka hadi wash room akaswaki alafu akamrudisha ndani akatenga kifungua kinywa akawa anamsaidia kula

" Kula sawa ili upate nguvu hata ukimeza dawa usijisikie vibaya sawa mama" Ikh aliongea kwa kubembeleza maana yeye mwenyewe anajua wagonjwa wanavokuwaga wasumbufu Naysha akawa anakula uku akiwa kafumba macho sasa Ikh si ndo akachota kijiko cha tambi alimsogeea mdomon tu Naysha alijisikia kutapika akamwambia hataka kutapika Ikabidi iki amsaidie jadi karibu na sink yaani alitapika nsizi zpte alizokul kosa tu ilikuwa ni zile tambi hakutaka hatak kusikia harufu yake,naada ya kutapika iki alimtoa akampeleka hadi bafuni ili aoge apunguze uchovu

" Naysha wewe ni mke wangu hata kama nilikuoa ndoa ya mkataba lakini bado wewe ni mke wangu naomba tuoge wote najua huwezi kusimama mwenyewe usigope sitokufanya chochote"aliongea Ikh kwa utaratibu sana akamvua nguo Naysha ya yeye akavua akaweka maji  ya vuguvugu kwenye jakuzi akashika Naysha taratibu akaingia naye kwenye yale maji yaliyoxhanganywa na shower jelly uenye harufu nzuri sana,alitangulia kukaa yeye akafuata Naysha akikuwa kafumba macho kwa kuhisi kizunguzungu muda wote akakaa na alivokaa tu basi Ikh alimkumbatia akaegemea pembe moja wapo ya jakuzi akamvuta Naysha akamlalia kifuani basi

kila mmoja alitulia kimya kama hakuna mtu Ikh alikuwa kafumba macho amemkubatia Naysha anampapas taratibu kabisa naye Naysha alikuwa kashikiria mikono ya Ikh amekaa kimya sasa ni pumzi zao tu ndo zilisikika, walikaa zaidi ya nusu saa kwenye jakuzi na baada ya hapo sasa ndo walioga Ikh akambemba Naysha akamrudisja chumbani akamtafutia na nguo akampa akavaa,akamuaga kuwa anaondoka kwwnda kwa rafiki yake atarudi baadae ye apumzike tu.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
whatsapp: 0687758688

Sehemu: 07 ($2)
Tulipoishia......
basi baada ya Ikh kutoka pale nyumbani alienda moja kwa moja kwa rafiki yake wa nguvu Fatih alipofika walikaa qakaanza kupiga story mbili tatu kama marafiki lakin mwisho Ikh alihitaji msaada wa mawazo sasa
" Ujue nini jamaa angu me kuna kit sikielew" aliongea Ikh
" Kitu gani hicho tena maana nawe siku hizi una mambo mengi kweli"
" yaani sasa hivi navokwambia ikitokea nikaambiwa nichague nampenda yupi aisee nitabaki njia panda yaani sijui kabisa"

"We ndugu yangu una changamoto sana kwani kimetoke nini hadi unasema hvo?"

" Yaani mwanangu juzi apa Naiphat alinipa dawa flan kwa kufosi nilale naye lakini sijui kwanini yaani katika wanawake wamenitoka basi ni Naiphat japo nampenda lakini naona kinyaa kushiriki naye tenda sasa alivoniwekea daw mawazo na akili yangu yote ilinituma tu kwa Naysha"

" Enheeee ikawaje?"

" Sasa baada ya kutoka pale nilienda moja kwa moja hadi chumbani kwa Nay jamaa angu ni aibu yaani ni aibu kabisa kule ni kubaka japo kwenye uhalisia sijui kwanini siku hizi najiskia amani sana kuwa karibu na Naysha kuliko hata Naiphat ambaye ndo nampenda"

" Ani we jamaa angu kwa namna moja aman nyingine naweza sema weww ni fara kweli yaani mpaka hapo bado hujajua tu kuw unampenda Naysha kuliko hata Naiphat?"

" Apana bhana me simpendi Naysha me nampend Naiphat"alibisha Ikh

" Aya endeleza kiburi chako na ipo siku icho kibuli chako kitakuja kukufanya umpoteze Naysha mazima na tena ukumbuke kilichokuwa kinamshikiria sana ni baba yake nacsasa amepona kuwa makini" rafiki yake alimpa tahadhari mapema kabisa ili asije akajutia baadae

Alimwambia rafiki yake yeye hawezi kuja juta hata siku moja

Basi alirudi nyumbani akaendelea kumtunza mke wke huyo wa mkataba na Naiphat alikuwa anakasilika kweli lakini hakuwa na namna akajifanya tu mstaarabu,kula walikula wote huku Ikh akimbmembeleza Naysha aliyekuwa anachagua vyakula kuwa ajitahidi kula ila anywe dawa, kama wakikaa sebleni basi Ikh angemwambia Naysha alale aweke kichwa chake lwenye miguu yake, kuoga walioga pamoja maana muda huo Naysha hakuwa naweza kabisa kusimama muda mrefu akiwa mwenyewe na kaka yake Nash alipiga sim kumjulia hali akamjibu tu anaendelwa vizuri ila alimuomba ombi moja tu amtafutie bana yake makazi maana angeruhusiw toka hospitali muda

wwote.

Zilishapita siku tano lakin hali ya Naysha hakuwa sawa hata kidog na hizo siku zote Ikh hakwenda kazini aliwajibika kwa kuamini ni ujinga wake mpaka ammemfanya Naysha kaumwa bila kukua kuwa huyo mwenzake ni mimba changa ndo inayomsumbua, ikabidi Ikh amuombe mama yake aje kumchukua Naysha akamtunze mpaka atakapopona Mama mkwe na anavompenda Naysha basi alikuja akamchukua Naysha akaenda naye kwake lakini yeye kama mtu mzima baada ya kumuangalia Naysha vizuri aligundua kit

" Naysha wanangu em niambie ukweli una shida gani?"alionge mama yule akiwa kamkazia macho Naysja ambaye hadi alihisi aibu

" Amna kitu mama mbona" alishindwa kumalizia kuongea kwa aibu  akainama chini

" Niambie tu ukweli mwanangu mimi ni mama yalo una mimba ety?" mama yule alivoongea hivo Naysha alitamani hata ardhi ipasuke aingie aisionekane

"Ndiyo mama" ilibidi aseme ukweli yaani baada ya yule mama kujua kuwa mkamwana wake ni mjamzito aliamka akaanza kupiga vigelegele akawa anaimba kilugha Naysha akawa anamuangalia tu maana hakuwa na usemi

" Sasa kwanini hujamwambia mumeo naye ajue taarif njema kama hizi?"

"Apana mama we usimwambie Ikh mpaka nitakapomwambia mimi mwenyewe" Naysha hakutaka kabisa mumewe hiyo wa mchongo ajua kama Naysha ana mimba  maana anajua kabisa asingeamini hata kidogo.Basi baada y mama mkww kujua vile alijitahid ndani ya mwezi mmoja na nusu Naysha alikuwawa aawa kabisa na akamwambia sasa ni muda wako kirudi nyumbani kwako na siku hiyo walienda kufanya utra sound wakaambiwa mtoto hana shida na ana afya njema kabisa basi Naysha alijiskia vizuri.

Jioni ya siku hiyo ndo muda ambao Naysha alirudi toka kwa mama yake mkwe alipofila tu akanza kufanya kazin ndogo ndogo za pale nyumbani maana nyumba ilikuwa chafu hadi haitamaniki,sasa akiwa chumbani kwa mumewe anapanga vitu vyake vizuri akasikia vicheko vya watu si ndo ikabidi aktoke alivotoka tu basi alikutana na dada yake na Naiphat.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 08 ($2)
Tulipoishia.....

baada ya Naysha kushuka chini basi alikutana na Naishia dadacyake na Naiphat baada ya kumuona tu walicheka mpaka wakagonga Naysha wala hakuonyesha kuwajari akaendelea zake na hsafi

" Nilikwambiaje yaani uyu sokomoko ana kiburi kama nini hukuamini umeona hata hasalimia"aliongea Naiphat

" Labda wewe ndo humjui me namjua uyo toka akiwa bado anajinyea ana dharau alafu ukiangalia baba yake ni maskini sana hana chochote sijui hwa analingia nini mim hatavsimueleagi" alijibu Naishia na muda huo sasa Naysha alishachoka akawageukia

" We Naishia unapokuja wenye nyumba z Watu jitahidi kuwa na heshima haupo kwa Bruhan hapa" weee alivoongea hivo ni kama aliwatibua

" Unasemaje wewe ayo maeno yako ya kijinga kawaambie watu wengine na ukome kumtaja mume wangu au unafikiri sijui kama umeolewa ndoa ya mkataba unaweza ukaachwa muda wowte unajsiahau sana ni bora hata mimi ndoa yangu ni ya ukweli na tunapendana" aliongea kwa kujinadi

" ni bora ndoa ya mkataba lakini amnaishi kwa amani kuliko ndoa ya halali kwa wapumbavu flani wasaliti na wezi wa wanaume za watu ambao wana mashaka muda wote" aljimjibu Naysha kisomi tena akachela lwa dharau sasa wakati wanaendelea kubishana nje kulisikia muungurumo wa gari kumaanisha kuwa Ikh alishatoka kazini anakuja nyumba,Naysha alivowajibu vile akaona haina haja kubishana nao muda mrefu sana akaona ni bora apande zake juu akapumzike sasa kumbe Naiphat na Naishia hawakuja kwa wema walishajua muda wowote Ikh anawwza ingia ndani alichokifanya Naiphat alianza kupanda ngazi kwa kasi sana hadi akamfikia Naysha alivofika akamng'ang'ania

Naysha mkono kila Naysha akiwambia niache anasema sikuachii sasa akavuta mkono kwa nguvu ilikwa ni kosa kubwa sana kwan Naiphat alijifanya amesukumwa na Naysha akaanza kushuka kwa ksi kwa kubiringita toka juu hadi chini sasa kama bahati mbaya Ikh pia aliona na kwa haraka unaweza his kweli Naysha alimsukuma mwenzake lakin haukuwa ukweli, alitua chini basi damu zilikuwa zintilikika maeneo ya kichwani kuonyenya kuwa kuna sehemu amechanika Ikh alikimbia haraka akaanza kujaribu kumuamsha kama ataamka lakin hakuamka Naysha kwanza alikuwa bado ameganda maana hakuelewa ilikuwaje mpaka mtu akawa chini namna ile baada ya kutoka kwenye

bumbuwazi ikabidi naye awakimbilie pale kuona nini kinaendelea alipotaka kumshika naifati alikula kofi moja takatifu sana toka  Kwa Ikh likafuatia lingine toka kwa Naishia

" Unataka umuue mwenzako wasababu ya wivu wako wa mapenzi kwani mwenzako alikwambia nini kibaya kama hupendwi si undoke kwanini uafosi sana mambo" aliongea dada yake kwa sauti ya ukali machozi ya uongo na kweli yakamtoka

" Sikuwahi kufikiri kama wewe mwanamke una roho mbaya kiasi hichi mimi nilishakuambia sikupendi kwanini unanilazimisha jamani? sasa ole wako Naiphat asiamke na kwambia kama sijakuua utahama hii nyumba" hayo yalikuwa ni maneno ya Ikh  alivomaliza hakugeuka nyuma akambeba Naiphati wakaongozana na Naishia hadi kwenye gari njia moja kwenda hospital

Baada ya kufika hospitali walipokelewa na Naiphat akaanza kupatiwa huduma baada ya masaa mawili aliamka basi alivoamka ilikuwa ni kilio tu

" Ikh unaona kila nikikwambia yulr mwanamke wako huwa ananione mara mara huwa huamini umeonacsasa kwani mimi nilimkosea nini?" hakumaliza kuongea akaangua kilio hicho ikabidi Ikh ambembeleze wakati huo

" Usilie bhana Naiphat nyamanaza utakuwacsawan a mimi najua jinsi ya kudeal na Naysha" aliongea hivo akataka kuondoka arudi nyumbani Naiphati alimng'ang'ania kwa kudai kuwa anaogopa hivyo anaomba alale hapo Ikh akakubali,Naishia aliaga akaondoka zake maana ilishakuwa usiku sana.

Asubuhi kabisa mida ya saa moja na nusu kaenye wodi ya  VIP aliyokuwa kalazwa Naiphat basi aliingia Naysha baada ya kuingia tu kwanza alichokiona kilimkatisha moyo sna alikuta Ikh amemshikilia Naiphat mkono alafu amelala kwenye kiti,mwanzo alivomfanyia vile alijua laabda anampenda sasa leo ndo alithibitisha kuwa anayependwa si yeye ni  Naiphat huenda kipindi kile alifanya vile tu kwasababahu alijua kosa ni lake. Basi hakuwaamsha aliamua tu kukaa pembeni kimya  mpaka walipokuja kuamka wenyewe

" Umekuja saa ngapi apa kwanza nani alikwambia uje hapa mpumbavu wewe" Ikh yaani hata bila salama alianza maneno yake ya karaha hapo sasa ndo Naysha akajua kabisa uyo aikh jawezi kubadilika ata siku moja

" Nilileta uji kwaajili ya mgonjwa" alikngea Naysha lwa upole

" Yaani Naysha me nilikukosea nini mpaka ukanisukuma vile je ningekufa? babe me nataka aniombe msamaha kama hatokubali me nitampeleka kituoni siwezi kukubali kabisa" alikngea Naiphat akaanza kujiliza.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688
sehemu: 09 ($2)
Tulipoishia......
Basi Naysha alipoambia achague aendw kituoni au aombe msamahan aliona mambo yasiwe mengi yeye siku zote hajawahi kuwa na thamani hata kidogo alipiga goti chini lakini wakati anapiga goti hadi chozi lilidondoka chini maana hakuwa amefanya kosa lolote
" Naomba nisamehe ni makosa yangu mimi kukusukuma kwasababu ya wivu wangu"aliongea vile Naysha akiwa anatilililikwa na machozi huku Naiphat akaonyesha tabasamu la dharau maan Ikh alikuwa amejiinamia hakutaka kabisa kuona jinsi Naysha anavyopiga magoti

" Kama kweli unataka nikusamehe basi naomba unitunze hadi ntakapopona" aliongea hivyo  Naiphat na Naysha akakkubali baada ya hapo akawakabidhi uji alafu akaambiwa arudi nyumbani kuweka mazingira vizuri maana jion ndo wanaruhusiwa, Naysha alitoka pale akiwa amelegea viungo vyote vya mwili lakini siku hiyo alimkumbila sana bana yake

" Baba shikamoo" alisalimia baada ya simu kupokelewa

" Marhaba hujambo mwanangu" aliuliza bana wa Naysha mzee Isihaka Baada ya kuuliza vile Naysha alishindwa kujibu akajikuta tu bila kutarajia amenangu kilio baba yake akamuuliza

" Shida nini mbona unalia binti yangu unajua baba hapendi kuona machozi yako?" aliuliza hivyo akijaribu kumtuliza Naysha asilie

" Baba nimechoka sana mwambia kaka Nash aandae chumba kwaajili yangu sasa nataka kurudi kukaa na wewe" aliongea Naysha na baba yake hakutaka kumhoji kwanini maana alijua kabisa binti yake anapitia kipindi kigumj hivyo alichomwambia asijali kila kitu kitakuwa sawa.

Jioni sasa ndo ulikuwa muda ambao mgonjwa alitolewa hospitalini na kuletwa nyumban basi alivokuja muda wote ilikuwa ni kumpeleksha tu Naysha mara nataka ichi mara icho sio yaani Naysha mpaka muda wa kulala basi alikuwa amechoka kweli kweli maana alisumbuliwa vya kutosha.

Zilipita siku mbili siku hiyo Naysha akaomba kuongea na Ikh basi walienda kukaa bustanini

" Ikh samahan najua nitakosea kwa nitakachokwambia nadhani sasa mambo yako yako sawa mwanamke unayempenda tayari yuko mikononi mwako naomba unipe taraka ili uwe huru kumuoa unakpenda maana anona labisa jinsi ninavyokubana" Naysha alitegemea kwamba labda taarifa ile ingekuwa njema kwa upande wa Ikh lakin kwenye halisia haikuwa hivyo ikh alikunja sura sana

" Kwani hapa kuna kitu unakosa mpaka unataka upewe taraka?" aliuliza Ikh akiwa kakunja sura

" Apana hakuna niachokosa ila tu nimechoka  kukaa hapa na uliniahid itakapofika miezi sita basi tutaachana na mimi nataka kuwa huru sasa" Naysha baada ya kuongea vile Ikh alijisikia vibaya sana na kuamini kuwa kumbe Naysha hampendi ndo maana anstaka uhuru kumaanisha kuwa anamwaume wake ambaye anampenda alijisikia vibaya sana alichokifanya akamwambia tu
" Sawa nitakupa iyo taraka unayotaka ila tu subiri nipunfuze ubize kwanza" alivoongea hivo Ikh hakutaka hata kusubiri jibu wala swali lijgine maana aliamni atazidi kukasilika tu.

Alipotoka pale aliendа kujifungia lwenye chumba na wageni alidondosha chozi bila kutajia mwanaume maana hakuamini kama kweli Naysha hampendi kiasi hicho na Naysha naye uku vile vile baada ya Ikh kutoka pale aliangua kilio cha hatari maana kwenye kweli alikiwa anampenda sna mume wake japo ni mwa mchongo lakin alimpenda sasa kupewa jibu kavu bile kuwa nitakupa ilimuumiza sana na akaamini moja kwa moja kuwa Ikh hajawahi kumpenda hata kidogo,alitoa simu yake akampigia Nash

" Kaka Nash uko salama wewe na baba?" aliuliza Naisha baada ya simu kupokelewa

" Ndiyo sisi hatujambo vipi wewe mzima" aliuliza Nash

" Ndiyo kaka ila siku yoytw kuanzia kesho tegemea kunipokea" alivoongea hivo aliangua kilio akashindwa hata kuongea alikata tu sim akaitupa uko kwenye majani akarudi ndani kulala.

Kulivokucha asubuhi Naysha alichelewa sana kuamka alikuja kugongewa na mgonjwa

" Amka bhana mumeo kaniachia karatasi ya taraka kasema usaini maana yeyey hatamani hata kukuona" ilikuwa ni sauti ya Naiphat baada ya Naysha kusikia vile basi alijicheka mwengwwe tu na kujiona mpumbavu.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 687758688

Sehemu: 10 ($2)

Tulipoishia.....

Baada ya Naiphati kumgongea Naysha mlango na kumwambia afungue asaini talaka Naysha alijicheka mwenyewe na kujiona ni mpumbavu kati ya wapumbavu wote duniani

" Ivi mimi nina akili sasa jana nilikuwa nalia nini ivi najisahaulisha wakati niliambiwa kabasa ndoa ya mkataba nilikuwa nategmea mwisho wa siku kuapta nini kama sio talaka em niache ujinga nafaa kurudi kwetu mimi sistahili upendo wa mtu yoyote na haya ndo maisha yangu" aliongea Naysba mwenywwe kisha akanyanyuka taratibu kabisa akaenda kufungua mlango akakabidhiwa talaka akakagua vizuri akajua kabisa ni talaka akadondosha saini akamkabidhi Naiphat

" Vipi nikupe nauli maana najua una muda hujaenda kazini so kwa vyovyote vile utakuwa huna hela" aliongea Naiphat kwa dharau

" Apana asante haina haja"alijibu Naysha

" Umepooza mwenyewe lakin ukumbuke mara ya mwish nilikwambia nini,nilikwambia Ikh hawezi mpenda mwanamke mwingne tofauti na mimi si kwa ubaya lakin safari njema shoga angu" aliongea hivo Naiphat akacheka alafu akageuka na kuondoka zake,Naysha baada ya hapo aliingia akaoga vizuri akavaa gauni tu fupi ya mwendo kasi maana mimba ilikuwa na miezi mitano na ilishaanza kuonekana kabisa lakini Ikh hakumshtukia,alipanga vitu vilivyomhusu alivomaliza alichukua karatasi na peni akaandia page nzima alivomaliza akaweka majibu ya ujauzito pale na karatasi ycutra sound hapo kisha akabeba mabegi yake  akapanga kila kilicho chake akakandamiza ile

barua na kitu kizito ili isipeperuke,alipofika getini akamwambia Moze

" Mozee kwaheri bhana mungu akipenda basi one day tutaonana"aliongea hivo akiwa na huzuni sana

" Daah pole sana Naysha yote maisha tu usijali naamini kila kitu kitakuwa sawa"aliongea hivyo moze na Naysha akatoka pale alivofika nje kaka ake Nash alifungua mllango wa gari na kumwambia aingie  ye akabeba mabegi yake akayaweka kwenye boot akaondoa gari maeneo yale.Sasa kumbe wakati wao wakiwa wanaondoka Naiphat alifanikiwa kuwapiga picha maana aliwaona na akaona kabisa apo ni ushindi kabisa.

Jioni ndo muda ambao Ikh alitoka kazini akarudi nyumbani sasa baada ya kufika alitegmea atakuta ata chakula lakini alikuta pakavu na Naysha hakuonekana kuwepo muda huo Naiphat alikuwa kalala hivyo hakutaka kumsumbua alitoka tu nje kumuuliza Moze kama alimuona Naysha

"Mozee umemuona Naysha akiwa anatoka?" aliuliza Ikh baada ya salamu

"Daaaah boss katika vitu ambavyo umefeli basi ni kumuacha Naysha aondoke mikononi mwako nakwambia hutokuja kupata mwanamke kama yeye broo wanawake kama Naysha kwenye dunia yetu wanahesabika"alitoa lawama zake bila hata kueleza nini kilitokea

" Ujue sijakuelewa bado nini kilitokea hadi unanambia hivo na nini kinaendelea"aliuliza Ikh akiwa haelew

" Boss iko hivi Naysha hayupo tena hapa namaanisha ameondoka na mabegi yake yote kumaanisha hatorudi tena hapa" aliongea Moze akaweka kituo

" Ujue Moze me sikuelew utasemaje hivo wakati unajua kabisa yule ni mke wangu"aliongea Ikh kwa ukali utasema Moze ndo alimwambia aondoke

" Boss we unafeli sana tu hujui hivi mambo mangapi umemfanyia yule mwanamke unafikiri wanawake wote wanaweza kuvumilia,lakini yeye amekuvumilia huoni hata haya kuniuliza hivo mimi kwakweli boss unakera kama ukikasilika kwa maneno yangu hata kazi nifukize tu me siwezi kufanya kazi kwa mtu mwenye moyo wa chuma usiohisi maumivu wala huruma"aliongea hivyo Moze na kwa mara ya kwanza alimjibu boss wake vibaya na akaondoka bila hata kugeuka nyuma,Ikh kwasababu kwa wakati huo alikuwa na hasira alitaka hata kumfata akampige maana aliona kama ni dharau kwa kiasi fulani,akatoka haraka hadi ndani akamkuta Naiphat kakaa akiwa

kashikiria kalatasi mkononi
" Leo umeshinda nyumbani uliona ni wapi alipoelekea Naysha?" aliulza Ikh bila hata salam wala kumuuliza anaendeleaje
" Babe mara nyingi sana nimekwambia yule mwanamke ameolewa na wewe kwa faida ona sasa shika hii ujionee mwenyewe" aliongea Naiphat akampa Ikh karatasi zilizokiwepo mikononi mwake Ik baada ya kuzishika ma kusoma zile karatasi yaani alihisi hasira akaanza lutetemeka ilikuwa ni karatasi ya talaka

" Kwahiyo aliona akisubiria kwa muda atachelewa sana kaona anipe talaka mwenyewe kumbe hakupenda namna hii"aliongea Ikh akiwa kama kachanganyiki akasimama kabisa akawa anaenda mbele anarudi nyuma anarudia kuangalia zile karatasi hadi jasho lilianza kumtoka Naiphat aliamka akaenda kumkubatia kwa nyuma

" Babe hakuna mwanamke anayekupenda kweli isipokuwa ni mimi tu Naysha alifata hela tu na dada ake aliniambia tabia nyingi sana za Naysha ni muhuni sana na huwa anawatumia wanaume wengi nakuwaacha kama ambavyo kakuacha wewe" aliongea Naiphat kuendelea kupigilia msumari

" Basi naamini sasa uko huru kipienzi saini tu hiyo taraka na unioe mimi ninayekupenda kwa dhat"aliongea hivo akitrgemea labda atashangiliwa lakini Ikh alimtoa mikono taratibu akamgeukia na kumwambia

"Niache siko sawa naomba nikapumzike na sitaki usumbufu"aliongea Ikh akapandisha juu chumban kwake akafunga kabisa mlango.

Tukutane sehemu ijayo.BE WITH YOU..2.11-15

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 11 ($2)

Tulipoishia.....

Ikh aliingia chumbani kwake akafunga kabisa na mlango maana hakutaka usumbufu wa aina yoyote.Naiphat alimpigia sim shoga yale Naishia

" Nikwambie mwenzio mambo yamejipa hatimaye nimefanikiwa kumtoa yule nyang'au humu ndani saivi niko mwenyewe utawala tu" apiongea hivo kwa fulaha maana aliamni ameshamaliza kila kitu yaani hapo kaweza

" Usijisifu sana huo muda unaotumia kujitapa kwangu ungeutumia kumfariji ili awe upande wako acha ujinga wewe mambo yanaweza badilika muda wowote"aliongea Naishia

" Sawa shoga yangu kesho"aliongea akata simu upande wa pili baada ya simu kukatwa Naishia alionekana kuchukia sana akatupa simu yake uko

" Pumbavu me nilitaka nyie wajinga wote mfeli ili mimi niingilie hiyo game kati maana namtaka Ikh kwa namna yoyote ile ila mmeharibu plani yangu"Aliongea hivyo kwa hasira sana kumbe hata si Rafiki ambaye unafaa kumtegemea ni mnafki tu maana yake hana urafiki wowote wa kweli kwa Naiphat ila anampa plani ambazo anajua akivuruga akashtukiwa basi atatimuliwa.

Upande wa pili Naysha alionekana club akiwe yeye,Nash rafiki wa Nash na mpenzi wake wenzake walikuwa wanakunywa pombe ila yeye aliomba tu juice

" Ujue nini rafiki yangu usijali sana em fanya kama hakuna kilichotokea fanya hiyo ilikuwa ni ndoto mbaya tu na imeshapita tayari em angalia una mimba sasa unampa huzuni hadi huyo mtoto" aliongea yule binti baada ya kumuona Naysha katulia hafanyi chohcote wanamuita haitiki yaani yupo kama hayupo hivi

" Ujue nini Suzie kitu kimoja mimi kinanichanganya ivi huyu mtoto akizaliwa nitamwmambia nini nawezaje kusema nilimzaa yeye kwenye ndoa ya mkataba na baba ake hawezi kumtambua?"aliuliza Naysha lwa huzuni sana

" Usijali sana hayo yana muda wake em jari afya yako kwa sasa hupaswi kuwa na stress"aliongea Suzie

" kaka yako niko hapa hupaswi kuwa stressed sana every thing done with a reason" aliongea Nash akaenda kumkumbatia Naysha na kumwambia

"Feel free to be with us your my blood younger sister"aliongea Nash na kudai kuwa yeye ni mdogo ake wa damu hivyo awe huru, Basi Naysha alimkumbatia kaka ake wa hiari akafumba na macho kabisa akakaa kimya akawa anasimiliza sauti ya kamziki kanakosikika lwa mbali kimya kimya.

Kulipokucha asubuhi basi Naiphat aliamka akaandaa kifungua kinywa anachojua yeye lengo likiwa ni kuvutia umakini wa Ikh na asiwaze  kuhusu Naysha,Ikh aliamka kw kuchelewa maana siku hiyo aliamua kujipa off maana hakuwa sawa hivyo alihitaji muda mrefu sana wa kupumzika.

Alipofika seblen basi alikuta kifungua kinywa kikiwa tayari  basi alikaa mezani ili apate kifungua kinywa lakini vitu alivyokutana navyo aisee alishindwa kula aacha kabisa maana kifungua kinywa hakikuwa kwenye Quality kabisa hivyo alishindwa na kunyanyuka kabisa akaenda kukaa seblen ndo muda huo akatoka Naiphat

" Babe umekifurahia kifungua kinywa?" aliuliza Nai kutegemea comment nzuri toka kwa mpenzi wake huyo ambaye bila kutarajia alijibu kawaida tu

" Cha kawaida tu na usijisumbue sana nitakuwa nakula hotwlini" aliongea Ikh hivo ili kukwepa tu kula vyakula vya ajabu maana kwenye uhalisia Naiphat hajui  kabisa kupika

" Okay babe kuna kitu nataka uone jana alichofanya Naysja yaani baada ya kutoka tu nje ya geti alifatwa hapo nje na benz kali kweli na mwanaume wake mzungu ona"alionge hivo akamuonyesha picha kuanzia  Naysha anafunguliwa gari,mabegi yake yanawekwa  kwenye boot hadi wanaondoka Ikh alisikia hasira,akaamka akaondoka bila kuongea chochote.

Ikh alitoka moja kwa moja akaenda kwa Fatih maana ndo nalikuwa mshauri wake mkuu  alipofika aliomba kwanza kulala baada ya lisaa limoja ndo akaamka

" Najua yamekufika shingoni niambie nini tena" aliongea Fatih akimsogezea maji maana macho yalikuwa mekundu kweli

" Fatih sijui  nifanyevnini nimechangsnyikiwa Naysha ameondoka na kaniandikia talaka me nimemksea nini"alilalamika Ikh

" Sasa wewe unalalamika nini mara ya mwisho si ulinambia humpendi wewe?"aliuliza Fatih

" Hata kama simpendi lakini mimi sitaki aondoke  nataka niwe namuona  muda wote" Ikh alijikuta anaongea ukweli ambao amekuwavakiuficha hata kwa Naysha

" Nafikiri sasa uko huru si ulisema unampenda Naiphat wapigie nyumban uwaambie mmeachana ili umuoe unayempenda" aliongea hivo Ikh akamuangalia kwanza

" Sidhani kama nataka kumuoa Naiphat sina hisia naye tena" aliongea Ikh lakin Fatih akampotezea tu.

Tukutane sehemu ijayo.Simulzi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 12 ($2)

Tulipoishia.....

Ikh baada ya kutoka kwa Fatih aliingia bdani akalala na aliomba asisumbuliwe na mtu  na ni kweli Naiphat sababu alikuwa kama anataka tuzo basi alikaa tu kimya.

Ndani ya mwezi mzima Naiphat alijitahid sana kujilengesha kwa Ikh lakin katika vyote alivovifanya hakuna ambacho kilifanikiwa hata kimoja yaani alionekana sijui vipi maana Ikh alivokuwa anatoka kazin basi alipitiliza ndani na kulala Naiphat akijalibu kumgongea basi angeambiwa hataki usumbufu.Na siku hizo ndo Naysha alikumbukwa sana maana Ikh alitamani basi akitoka kazini basi hata aulizwe umeshindaje? siku yako imeendaje? chakula kiko tayari,nguo nimeshakupasia lakini katika vyote hivo hakuna alichokipata yaani al8taman hata amtafute Naysha lakini alipopiga simu yake haikuwa inapatikana na mlinzi aliishia kumletea simu ya Naysha kisha akamwambia

aliikuta ikiwa imetupwa bustanini,Ikh alijisikia vibaya sana na kuamini kuwa Naysha hakuwahi mpenda ata kidogo na ndo maana hata alivotkaa kuondoka aliacha hadi simu ili asisumbuliwe na kilichomsiktisha zaidi aliambiwa kuwa alifatwa na mwanaume wakd mzungu basi aliamini kuwa Naysha alikuw anamtumia kwa manufaa yake. Basi alijikuwa kila siku anajitahid kumsahau lakni ilikiwa haiwezekani.

Ilikuwa siku ya jumatatu Ikh akiwa kazini lakini hakuwa sawa basi alipigiwa simu na mama yake akapokea
" Shikamoo mama" alisalimia Ikh

" Unahisi me nataka hata shikamoo yako we mtoto?" alijibu ivo mama yake Ikh na kumfanya  ikh ashangae maana toka anakua hajawahi sikia mama ake akiwa mkali ivo tena kwake.

" Mama kwanini unasema hivo kuna kosa gani nimefanya?" aliuliza Ikh akiw na wasiwasi alihisi kuna kitu kibaya kimetokea

" Unauliza kitu gani kwani hujui unawezaje kumuacha Naysha ndoa yenu ikiwa haina hat mwaka ni kosa gani kubwa amelifanya kwako hadi umeshindwa kumsamehe mpaka umeona umpe talak?" aliuliza mama huyo kwa hasira

"Mama sikiliz Nikwambie" ikh akiwa anataka kujieleza mama yake alimkatisha

" Nisikilize nini hivi unajua Naysha kwasasa anapitia kipindi gani? hivi uliwezaje kumuacha mwanamke akiwa na mimba kkabisa tena inayomsumbua?" ile taarifa kwa Ikh ilikuwa ngeni kabisa maana hakuwa anajua kabisa kama hata Naysha ana mimba

" Maa unasemaje? nani anamimba?" aliuliza Ikh akiwa anatililikwa na jasho kama maji maana ile taarifa ilimshtua kuliko zote

" Naysha amekuwa akihangaika na mimba yako muda na sasa hivi hiyo mimba ina miezi sita lakini hujali kuhusu yeye unajali mwanamke wa nje kweli Ikh? hayo ndo malezi tulokulea sisi?" aliuliiza mama yule kwa uchungu akakata na simu maana alijisikia uchungu sana alipofikiria kuhusu maisha ya Naysha na jinsi mimba yake ilivyokuwa inamtesa na hajui mpaka muda huo yuko wapi na anaishi vipi

Ikh alitoka pale akiwa speed sana alifika nyumban akamkuta Naiphat kalala seblen maana kwa kipindi hicho Naiphat hakuwa anaenda kazini hivyo alivyofika alimuamsha

"unaweza niambia siku ile Naysha aliondokaje na ilikuwaje akakuachia kalatasi ya talaka?" baada ya Ikh kuuliz Hivyo Naiphat kidogo alionekana kuchanganyikiwa kidogo na alitoa majibu ambayo kwa upande wa Ikh hakuyaelewa hata kidogo

Alitoka pale wazo lake lilimtuma kwenda kwenye chumb alichokuwa anakaa Naysha maana toka ameondoka hakija wahi kufunguliwa,baada ya kuingia kwenye chumba kile alisimama kwanza akaanza kumkumbuka Naysha alikumbuka jinsi walivyokuwa wanalala pamoja kweli kabisa alimmisi sana alitaman hata kumuona  Aliangalia picha ya Naysha ambayo aliisahau ukitani basi alikuwa amekaa kwa utulivu kweli lakini alipotupa jicho mezan alikuta kuna karatasi zimekandamizwa na cable akabidi azisogelee kwanza juu kabisa alikutana na karatasi ya utrasound na ya pili ilikuwa barua akaona asome barua kwanza.

Je kwenye ile barua kumeandikwa nini?

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 13 ($2)

Tulipoishia.......

Baada ya Ikh kushika ile barua aliamua kuifungua ili asome ndani kumeandikwa nini,barua ile ilisomeka hivi

" Habari Ikh,najua hii barua unaweza iona mapema au baadae lakin kwanz Kabisa napenda nikushukuru kwa kumsaidia bbaba yangu hadi sasa mzima kabisaa wa afya tele pia kunipa mahitaji yangu yote,kutokana na kujali kwako ilifikia hatua ulinifanya nikakupenda sana nikaamini naweza kukubadilisha na wewe ukanipenda lakini nilijidanganya hukuwahi nipenda,ulinitumia kwa nguvu bila hata kujali hisia zangu kuonyesha kuwa sikuwa wa thaman na nilikiwa kama malaya tu inaniuma sana pia nasikitika sana kuona kijana msomi mwenye ufahamu mzuri tu lakin umeshindwa kuona ukweli wa mambo umepumbazwa na mtu ambaye hakufaa

hata kupokea uaminifu wako,umenifanyia kila aina ya vituko na nikavumilia ,mwanamke wako pia ameninyanyasa sana,lakini nataka niapem mbele ya mwenyezi mungu ile siku mimi sikumsukuma Naiphat na kama unataka kuujua ukweli nadhani ndani kuna cctv unaweza angalia zitakwambia ukweli,pia nimethibitisha ichi kitu siku ya leo kuwa hukuwahi nipenda maana nimekuomba talaka jana na leo asubuhi ukaona huwezi vumilia kabisa adi urudi jion ukaamua kumtuma mwanake wako aniletee nisain ili usinikite kabisa,sawa nimekubali na nimshasaini kuanzia sasa uko huru na umpendae nakuahidi sitokuja kujitokeza kwenye uso wako na nitaenda mbali

ambako naamini hatutokuja kuonana na kuhusu ujauzito ukitaka kuamini ni wa wakwako sawa na usipo amini ni sawa nimeshajopanga kuwa single mama tayari nitamlea mwanangu na sitokuja kumwambia kuhusu wewe maana naamini hautofurahia kwasababu hutotaka mtoto aliyezaliwa kwenye ndoa ya mkataba pia alizaliwa kwa zao la chuki na si upendo,basi naamini kuanzia leo utaluwa na furaha kabisa na utapata watoto wazuri na Naiphat na mtawapenda sana,kuhusu simu niliitupa bustanini maana sikutaka kuondoka nayo ningekusumbua kwa hiyo nimeitupa kabisa ili nisije kukusumbua kwa upendo wangu wa kipumbavu na iyo picha juu ni utra sound yangu ya

mara ya mwisho ambayo nilipiga kuangalia kuhusu maendeleo ya mtoto nikiwa na mama ukipenda utaangalia pia usipopenda utaichana,kwaheri Ikh kuwa na furaha maisha yako yote" barua hiy ilisomeka hivyo ambayo mpaka Ikh anamaliza kusoma basi alikuwa ameshailoshewa ile barua machozi na alikuwa anatetemeka balaa alilia mwanaume maana hakuweza kustahimili yale maneno ya kwenye barua yalikuwa makali lakini yenyw ukweli mtup alijilaumu na kujiona mwanaume mpumbavu hajawahi tokea duniani,akichokifanya alibeba ile karatasi na picha ya Naysha akaenda hadi ndani alimpita Naiphat kama hamuoni moja kwa moja alienda kwenye

chumba chake cha kufanyia kazi basi aliwasha laptop yake akachomeka flash fulani ya kutunzia kumbukumbu za nyumban alivyoiweka aksearch ile tarehe ambayo Naiphat alidondoka akaipata video akaplay

aliona kila kitu kuanzia mwanzo wa tukio hadi mwisho yaani mpaka video ilipoisha basi alipigiza laptop chini maana alikuwa na hasira sasa hapo ndo alikuja kutambua jinsi gani yeye alikuwa mjinga na mgumu wa kitambua mambo akamhukumu Naysha bila hata kusikiliza maelezo yake akaonackwamba Naysha ana roho mbaya hajali kuhusu wenzake.

Alivotoka hapo aliendа moja kwa moja chumbani anapolala Naiphat na Naiphat alikuwa ndani kajituliza akashangaa mtu kaijgia kanyooka kwenye kabati akavuta begi juu akaanza kutoa nguo kwenye kabati anaweka kwenye begi ikabidi anyanyuke amuulize

" Babe mbona unapanga nguo zangu kwenye beg vipi tunasafiri ety?" aliongea kwa kujilegeza kwa akili yake akaamini kuwa huenda wanasafili wanaenda piknik

" Ngoja nimalize kwanza ndo utajua" aliongea Ikh akiwa busy kweli kupanga nguo na Naiphat akatulia kambisa pembeni akiamini ndo mahaba yanerudi

Baada ya kumaliza kupanga akaanza kuburuta begi hadi pembeni na Naiphat akavaa haraka akamfata nyuma akiamini ni safari sasa ndo inaanza, Walipofika seblen mpaka mlangoni akaona anasukumizwa nje

" Babe kuna nini tean mbona unanisukuma?" aliuliza Nai kwa ghadhabu maana alisukumwa kidogo adondokr

" Unataka kujua unaenda wap sasa unaona lile geti pale uloingiliaga kwenye hii nyumba basi ndo hilo hil utakalotokea siwezi kuishi na mwanamkr mpumbavu kama wewe ambaye uko tayari kuumiza watu wengine au kujiumiza ili kuharibu tu maisha ya mtu mwingine siwezi na nakuomba kuanzia leo tusisumbuane na nisikuone unakanyaga mahali hapa yaani lile geti pale lione kama jela kama sio jela basi lione kama kuzimu haya toka" aliongea Ikh kwa sauti apo ndo Nai alishtuka na kujua kuwa hawakuwa wanaenda piknik basi alijichanganya

" Lakin babe mimi nimefanyanye mbona sielew kosa langu nini?" naiphat aliongea akiwa kachanganyikiwa

"usijifanye kama hujii nini umefanya kwanini ulinidanganya kuwa Naysha ndo kakupa talaka unipe nisaini kwakati hiyo talaka wewe ndo ulipeleka kwa Naysha?" Ikh alivosema hivo sasa apo Nai akili ikafunguka na kujua kuwa Ikh tayari ameshajua kuwa alichezewa game

" babe nisikilize nilikusaidia wewe tu maana ulikuwa unataka kumpa talaka na kutaka kunioa mimi hivyo nikakusaidia babe sababu nakupenda" aoijitettea Naiphat

" Unajisaidia nilikuomba na ulivyo huna haya ukajindondisha na kumsingizia mwenzio unafikiri mimi nataka kuishi na mwanamke mwenye akili kama zako yaani najuta sana kukuamini wewe mwanamke mpumbavu" Aliongea Ikh akiwa anamsukuma Nai aondoke kwake maana alikuwa kila akitazama alihisi hasira sana

" Babe najua nilikosea lakini wewe kipindi hicho hukuwa na muda na mimi alafu mimi nakupenda sana, najua nilikosea lakini nilitaka tu tubaki mimi na wewe nakupenda sana" aliongea Nai akiwa anadondosha chozi

" Mimi siwezi kuishi na mwanamke mwenye tabia kama zao em toka apa bhana usije nitia hasora nikajikuta nimekuvunja mguu bure,moze njoo utoe hii takataka hapoa sitaki kuiona kabisa" aliongea Ikh na akamuita Moze ambaye hata hakumchelewesha alimburuta hadi nje akafunga na geti kabisa.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 14 ($2)
Tulipoishia.......

Baada ya Ikh kumfukuza Naiphat basi alimpigia siku rafiki yake na kumuomba aje nyumban kwake akajibu sawa,wakati akiwa amekaa kumsubiri Fatih aje basi alikuwa ameshikilia picha ya Naysha akiwa anaipapasa alikuwa analia kama mtoto mdogo na kujuta kwa ujinga alomfanyia binti wa watu bila hata kujali alilala naye kwa nguvu akampiga na kuruhusu Naiphat amnyanyase anavyotaka,kazi akamfukuza bila hata sababu maskini yaani alijuta kwa mengi

" Nisamehe Naysha najuta natamani nirudishe siku nyuma ili nirekebishe makosa yangu najutia kwa ujinga nilioufanya kwako,nakubali mimi ni mwanaume nisiye na moyo wa utu hata kidogo hata kidogo, niambie uko wapi Naysha nikufate? sijui una ishi vipi na mwanangu sijui unaendeleaje? mbona umenipa adhabu kubwa sana hivyo mama angu ungenisamehe basi usiende mbali na mimi nakupenda ety najuta kukupoteza mimi" hayo yalikuwa ni majuto ya Ikh na rafik yake Fatih alifika akamkuta Ikh analia kama mtoto uku kakumbatia picha ya Naysha alalia kweli ikabidi Fatih ashtuke kwanza kuna nini? au kuna msiba Naysha kafariki au kuna nini yaani aliwaza vitu vingi

kweli,akamsogelea Ikh na kumpokonya ile picha na kumpiga piga mgongoni rafiki yake huyo

" Pole bhana acha kulia we mtoto wa kiume" aliongea Fatih

" Acha tu nilie mimi ni mpumbavu sana ona ona Fatih nimemsukuma mbali mwanamke ninayempenda na ansyeweza kunivumilia mimi,angalia Naysha ameniacha mimi amenikesha Fatih sijui alipo kichwa kinauma,ameondoka bila hata kuniaga mwanzo nilikuwa na hasira nayekwa luamini yyeye ndo kanipa talaka maan nilikuta amesain bila kujua Niliingia lwenye mitego ya yule mwanamke mshenzi angalia Fatih sijui Naysha alipo?sijui mwanangu anaendeleaje kiburi changu kimeniponza na upofu wangu wa akili nimepompoteza mwanamke wa ndoto za kila mwanaume Fatih nisaidie nifanyaje" alikuwa anaongea Ikh akiwa kama

kachanganyikiwa
" pole bhana lakini kama unakumbuka nilishawahi kukwambia utakuja kujuta na kiburi chako kitakuponza utampoteza Naysha na itakuwa ngumu wewe kumrudisha tena kwenye mikono yako unaona sasa jeuri yako imekusaidia nini?"
" Najuta fatih natamani nirudishe siku nyuma nimuombe Naysha msamaha nampenda ety na sijui kama atanielwa vipi kihusu mwanangu nachanganyikiwa ety jamaa angu"
" Nimekusikia unataja mtoto ni mtoto yupi unamzungumzia?"

" Mwanangu Naysha aliondoka hapa akiwa na ujauzito,ona mara nyingi nilimuomba Naiphat anizalie lakin alinijibu yeye hataki kuharibu umbo lake la kimisi lakin yeye alibeba mimba yangu na hakuwaza kuhusu hilo nisaidie nifanyaje?"

" Duuuh hapo mtihani yaani Ikh umefeli pakubwa sana na ni kazi sana kumrudish Naysha tena mikononi mwako maana umemfanyia mengi ya ajabu hawexi kukuamini tena lakin ngoja tutajaribu kumtafuta tujue alipo" aliongea Fatih.

Naysha alikuwa amechoka kweli maana mimba ilishakuwa kubwa sana na ndani ya hicho kipindi basi  Kuna ukweli ambao aliufahamu kuhusu Nash akak yake wa hiyari, kumbe hakuwa kaka wa hiari bali alikuwa ni kaka yake kabisa ambaye baba yake alimzaa kipindi alivokuwa masomoni nje ya nchi baadaye wakaja wakagombana na mama yake akarud8 Tanzania na kumuachia  mama wa Nash kila kitu maana aliijwa na nyumba magari ambayo aliyapata akiwa huko marekan basi aliacha ndo akarudi kuja kuanza moja na ndo kipindi alichokutana na mama yake Naysha akiwa hana kitu zaidi ya kazi tu na walikaa kwenye nyumba ya kupanga,kuja kwa Nash

hakuja bure isipokuwa alikuja kumtafuta baba yake na baadae alikuja kugundua kuwa ana ndugu mwingine ambaye ni Naysja na ndo maana mara ya mwisho alimwambia yeye ni ndugu yake wa Damu hivyo Naysha aliambiwa ukweli huo na baba yake na Nash akamwambia kuwa mama yake anataka kuja Tz kuiishi nao kama tu baba ao atakuwa tayari maana tayri kuna vitu vingi alishajiwekeza tanznia ,mzee Iskihaka alikubari mwanamke wako huyo wa zaman aje tu waendelee kuishi pamoja na mpaka kufikia kipindi ich bas mama wa Ikh alikuwa anaishi nao kwenye moja ya majumba yake ya kifahari ambayo isikaha alipoangalia alikuta hati ina jina lake na alipomuuliza

alimwambia kuwa iyo nyumba ilinunuliwa na pesa ambazo alimuachia kipindi anaondoka marekani.Nasiaisha kwa upande wao yalikuwa mazuri na waliishi kwa upendo kweli yaani upendo ambao Naysha aliukosa toka kwa mama yale mzazi basi aliupata owa mama yake Nash ambaye ni kaka yake na Nash mwenyewe basi alikuwa anamdekeza mdogo ake hadi so vizuri.

Siku hiyo Naysha alikuwa na kaka yale Nash wakiwa wanafanya mazoezi na tumbo lake kubwa basi walikuwa wanatembea barabaran Naysha aliwambia kaka ake kuwa kachoka kutembea basi kaka yale alirudi nyuma akamshika mkono wakawa wanatembea taratibu sasa kama bahati mbaya njiani si wakakutana na Naishia

" Mmmh naona sasa wabongo wamekushinda umeamua kuhamia kwa wazungu shoga angu heeee hutaki kulaza damu jaman aya nitambulishe kwa shemeji" aliongea Naishia kwa dharua na cheko juu kabisa

" Uwage unapungiza mdogo da Nai so kila mwanaume unayemuona basi unamattack bila hata kuuliza utakuja kutolewa meno bure" alimjibu Naysha kaka ake akambia

" Don't talk to her yuko kama ana kichaa" aliongea Nash na kimshika mkono Naysha wakaanza kuondoka

" Waoneni vile na tutaona hayo mahusiano yenu yatafikia wapi" aliongea Naishia kwa wivu maana anakerwa sana kwanini Naysha ndo awe tu na wanaume wazuri wazuri maana mwanzo alijua kumchukulia Bruhan ndo kamkomesha lakin haikuwa hivyo lwan mambo yalizidi lumnyookea mdogo ake na sasa alijua amemaliza mchezo lakini kwa anachoamini yeye kuwa sasa hivi yuko na mzungu.

Jumanne asubuhi Naysha aliamka akiwa hajiskiii vizuri ikabidi kaka yake ampeleke hospitalin maana muda huo mama ba baba yao walifaa kwenda kazini hivyo walimuomba Nash amsindikize mdogo ake,walitoka na kwenda hospital sasa walipofika wakiwa wanasubiri kuonana na docta Nash akamwambia mdogo ake alale kwenye miguu yake,naye Naysha sababu alikuwa anajisikia vibaya basi alilala kaka yake akawa anambembelez kwa kuzishika nywele zake.Watu walikuw karibu yao waliamin kuwa wale ni mke na mume bila kujua kuwa hao walikuwa ni mtu na dada yake.Sasa wakiwa bado wamekaa pale saa ngapi Ikh asijr pale na kuwakutaxwakiwa wamekaa hivyo.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 15 ($2)

Tulipoishia........

Kwasababu Ikh usiku wa jana yake hakualala vizuri basi aliamka asubuhi na kuamua kwenda hospitali kidogo akafanye check up ya mwili wake maana alikuwa na muda kidogo kucheki afya ayake sasa alipofika pale ndo akakuta Naysha akiwa kalala m8guuni mwa Nash,roho ilimuuma akaamini kuwa tayari Naysha ameshapata mwanaume mwingne na kwasabahu ya ushenzi alomfanyia basi akajua moja kwa moja huenda Naysha asimsamehe maana amemfanyiavmengi mabaya aliingia tu kwa dokta kimya kimya bila kuwasemesha alivotoka hapo aliondoka na kwenda nyumban kwa mama yake moja kwa moja,Alipofika tu alimuomba mama yake msamaha kwanza alafu ndo

akaanza kuelezea hali halisi

" Mama yaani ninavokwambia hapa nimechanganyikiwa sijui hata ni nini nifanye Nayshavtauari yuko na mwanaume mwingine vipi kuhusu mwanangu mama na vipi kuhusu mimi mbona nampenda sana" aliongea Ikh kwa huzuni sana

" Ikh mwanangu umekosea sana yaani hata siku moja mwanaume hawezi waweka mke na mchepuko sehemu moja uliwaza nini mwanangu mpaka ulafanya hviyo angalia sasa ivi Naysha utamrudishaje tena mikononi mwako?" aliojgea mama yule na kumsikitikia mwanae ambaye ndani ya huo mwenzi mmoja basi alishaisha maana mawazo hayakumuacha salama

" Mama mimi sielewi mamawanzo nilkikuwa simpendi lakin nimekija kugundua kuwa mimi nampenda sana yeye na ni ngumu lwa upande wangu kuishi bila uwepo wake nashindwa mama sijui nifanyaje?" aliongea Ikh akitamani ata kulia

" Nakosa cha kusema maana kama mama nilishakuonya mara nyingi sana kuhusiana na suala la wewe kuwa mbali na yule mwanamke lakin hukunielewa mwanangu ona sasa umeharibu pakubwa sasa mimi nakusaidiaje mwanangu ?"

" Mama najua wewe ni mtu mzima naomba nisaidie miki nampenda sana mke wangu nataka arudi na nikimpata niko tayari kumpigia magoti na kumuomba msamaha hatacsiku nzima ilimradi tu yeye akubali kunisamehe" aliongea Ikh akiwa anatilisha huruma sana

" Basi sawa cha kwanza unachotakiwa kufanya lazima ujue kwanza anakoishia Naysha kwa sasa alafu mengine tutajua baadae"aliongea hivyo mama Ikh na ikh akaaga kuwa anarudi kwake kupumzika maana kichwa kilikuwa kinamuuma sana.

Upande wa Bruhan na mkewe Naishia amani haikuwepo hata kidogo maana kila Naishia alipofosi kubeba mimba basi Bruhan angemlwepa na kumwambia hayuko tayari kuzaa na yeye sababu yeye sio mwanamke wa ndoto zake waish tu

Hiyo hali ilimfanya Naishia akose amani sana na kuna muda alitukana sana na kumulaumu mdogo ake kuwa ndo chanzo hadi mwanaume hataki kuzaa naye na huenda hata ile mimba ya kwa Naysha ni mumewe ndo maana hataki kuzaa na yeye basi alitaman hata kumroga mumewe huyo ili tu atulie maana mume alianza kudate na wadada wengine hovyo bila hata kujali kama ana mke na alipomuuliza alisema yote kasababisha yeue ambaye alimrubuni mpaka akamuona maana yeyd hampendi anampenda Naysha,na baada ya Bruhan kujua kuwa Ikh kamuacha Naysha basi alijitahid kila awezavyo basi kumuweka Naysha upamde wake lakini

haikuwezekana,basi akachagua tu kuwa na wanawake tofauti tofauti.

Ikh alitumia week mbili kupafahamu anapoishi Naysha na alikuja kugundua kuwa Naysha anaishi tu maisha mazuri ambayo yanalingana na maisha aliyokuwa anaishi kwake pia alikuwa na kazi nzuri na baba ake alikuwa na kazi nzuri tu,apichunguza mpaka akajua latiba za Naysha na akamwambia mama yake kuwa Naysh siku hiyo basi al8takiwa kwenda clinic na ataenda peke yake  hivyo mama yake alienda kwenye hiyo hospital ambayo Naysha alikuwa anaenda kuangalia afya yake na ya mtoto,Naysha alivyofika pale hospital basi alikuwa kakaa anamsubiri Docta wake alienda kupata kifungua kinywa mara ghafla akshangaa anasalimiwa

" Hujambo mwanangu?" ilikuwa ni sauti ya mama Ikh ilomfanya Naysha ashtuke na kunyanyua kichwa na kipindi hicho alikuwa mzito kweli maana mimba ilishafikisha miezi saba hivyo alishaanza kuchoka sana.

Tukutane sehemu ijayo.BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 16 ($2)

Tulipoishia.....

Baada yA naysha kunyanyua kichwa basi alikutana na sura ya mama yake Ikh basi alishtuka kweli

" Shikamooo mama" alisalimia akiwa anakaa sawa

" Marhaba mwanangu za masiku?"

" salama tu mama vipi wewe ba baba mnaendeleaje?"

" Tunaendelea vizuri samahan mwanangu tunaweza kuongea?" aliongea mama Yake ikh kwa unyenyekevu

" Ndiyo mama usijali tuzungumze tu maana bado namsubiri docta" Aliongea Naysha kumtoa wasiwasi

" Sawa mwanangu vipi lakini maendeleo yako na mwanao?"

" Maendeleo tu mazuri sema ndo kama hivo kidog navimba miguu siju kwasababu ya nini lakin tuko vizuri"

" Mwanangu ivi unaweza niambia nini kilitokea mpaka  mkapeana talaka na mwenzio maana sielew na nikimuilza mwenzio hanipi majibu ya maana"

" Mama kiukweli kwanza nitangulize tu samahan huenda hata hili pia utakuwa hulijui mimi na Ikh tulikuwa na ndoa ya mkataba na alisema anafanya hivyo ili kuwaridhisha nyie ambao mlikiwa mnamsumbua kuona lakin hanipendi mimi na mimi nilikubali kwasababu aliahid kumtibia bbaba yangu na kunilipa mimi kiasi cha shillingi milion tano nikakubali sababu nilikuwa na shida sana hvio hata kipindi kile tulivyoenda honeymoon hakuna kitu chochote kilichoendelea,tuliigiza mbele za watu kuwa sisi ni wanandoa kweli laki  ndani kila mtu alilala chumba chake na mambo yalikuja kuwa magumu zaidi kioindi ambacho alikuja mwanamke wake maana nilinyanyaswa sana ila

kuna siku mwanamke wake alimwekea dawa flni kwenye kahawa ndo siku ambayo mimi nilibeba mimba maana hakutaka kulala naye alikuja kwangu na kulala na mimi kwa nguvu,kama Talaka nilimuomba mimi kwasababu

Nilishindwa kuvumilia vituko alivyokuwa anajifanyia nikaona tu nimuache hru yeye na mwanamke wake hivyo ndo ilivyokuwa mama angu"

" Daaaaah nyie watoto mna balaaa lakini mwanangu hivi ikitokea Ikh akakwambia  anakupenda na anataka mrudiane utakubali au utakataa na vipi wewe unampenda?"

" Mama msema ukweli mpenzi wa mungu mimi Ikh nilikuwa nampenda sana japo sikuwahi kumwambia lakini nilimpenda ila yeye jakiwahi nichukulia mimi kama mwanamke hanipendi mimi anampenda mwanamke wake mama na hilo wala hata halipingwi"

" Naysha mwanangu em usijiaminishe sana mimi ni mama wa Ikh namjua mwanangu toka akiwa mdogo Ikh kiburi ndo huwa kinamponza sasa unavyyosema hivo vipi kuhusu mtoto?"

" Kuhusu mtoto mama mimi nitamlea tu maana tayari nina kazi nzuri nina ndugu wanao nisapot nmsishindwi kumlea najua Ikh hawezi kukubali atahisi nimemsingizia mimba hivyo acha tu me nitamfsnya mwanangu peke yangu"

" Mwanangu hivyo unakosea huyo mtoto anafaa pia kupata malezi ya baba huoni kama unakosea?"

" Sion kama nakosea mama na kuhusu malezi ya baba kaka angu yupo atanisaidia tu haina tatizo nataman kumuona Ikh akiwa na furha na ndoa yake ijayo hivyo sitaki kumsumbua tena ndo maana sijawahi mtafuta"

" Ikitokea sasa mumeo anataka urudi nyumban utarudi?"

" Mama hiyo haiwezekan ikh hanipendi mimi hata akinirudisha basi itakuwa kwa shinikizo lako wewe mama hviyo nitaishia kuteseka tu na mimi hicho kitu ndo sitaki kabisa"

" Basi sawa mwanangu tutaendelea kuwasiliana namba yangu hii hapa" aliongea mama Ikh kisha akatoa busnesscard yake akampa Naysha ambaye aliipoea na kuweka kwenye pochi yake na mama Ikh akaondoka muda huo.

Naysha alipokuwa nyumban jion basi aoipigiwa simu na nba ambayo kwa kuingalaia tu basi alijua kabisa ni Ikh akakata hakutaka kujikumbusha machungu ambayo alishaanza kuyasahau taratibu lakin Ikh hakukata tamaa alipiga na kupiga tena hadi Naysha akaamua kupokea, baada ya kupokea Ikh alisikika akiwa analia

" Naysja mke wangu najua nimekukosea mamaa lakin adhabu uliyonipa ya kukaa mbali na mimi inatosha mke wangu em rudi nyumbani me nimemisi kukuona mke wangu ukichelewa me nitakufa nakuomba mama nisamehe mwenzio nimekoma" aliongea Ikh kwa sauti ya kilevi huku akiwa analia basi na kitu Naysha hawezi vumilia ni kumsikia Ikh akiwa anaongea kwa hzuni kama hivo alinyanyuka haraka sana akamwambia kaka yake Nash amsindikize nyumbani kwa Ikh kweli ata wazazi waliwaambia waende tu hivyo Nash alimpeleka dada yake hadi getini kwa Ikhram wakagonga geti lilivofunguliwa nasi Naysha aliwambia kaka yake huyo ambaye alikuwa na wasiwasi na Naysha kuwa

aende tu yeue atakuwa sawa hata asijali.Nash akaondoka na Naysha akaingia ndani yaani hata Moze alivomuona alishtuka maana hakutrgemea kama angeweza kurudi pale ndani lakini mshtuko wake ulichanganyikana navfuraha Naysha alimsalimia akampita akaingia ndani alipofika seblen basi alikutana na harufu ya pombe isiyo ya kawaida na Ikh alikwa amelala chini yaani alikuwa amelewa hadi hajielewii, Naysha alimsogelea

" Ikh amka mimi Naysha niko hapa nimekuja nyanyuka basi unitazame" aliongea Naysha akijaribu kumwamsha Ikh ambaye alikuwa anaongea vitu ambavyo hakuvielwa

" Umekuja Nay wangu mke wangu,sasa kwanini uliniacha na yule mwanamke nyoka mama kwanini hukuniambia mapema au basi mimi ni mpumbavu hata ungeniambia basi nisingeksuikiliza" alikuwa anaongea na kujijibu mwenyewe, Naysha alimuojea hruma ikabidi tu amkokote hadi chumbani kwake na akawa anajiuliza inakiwaje Ikh analewa vile na Naiphat  yuko wapi hadi muda huo,Waliodika chumbani basi amsaidia hadi wakaenda bafuni akamsaidia akaingia kwenye jakuzi akaweka maji ya baridi sana ili kidog akate ile pmbe alivotaka kutoka Ikh akamvuta mkono na kulamika kuwa hawezi kuoga peke yake hivyo akamvuta Naysha naye akaingia

kwenye Jakuzi na nguo zake hivyo hivyo,Naysha aliona tu amuache afanye anachotaka aliingia akakaa mbele yake alafu akamlalia kifuani,anampenda sana mwanaume huyo lakin njia zao hazifanani mwanaume hampendi yeye anampenda mwanamke mwingine hicho ndo kitu kilimchosha Naysha akili,aliona atumie muda huo basi kuilidhisha nafsi yake muda ambao Ikh alikuwa hajitambui hivyo alimlalia Ikh kifuan na kumkubatia vizuri japo maji yalikwa baridi ila kwake aliona sawa tu.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 17 ($2)

Tulipoishia.....

Naysha alimkumbatia Ikh vizuri alafu akafumba macho kabisa alijikuta anapitiwa na usingizi pale pale na ile hali yake ya uchovu wa mimba hakutumia hata muda mrefu aliuchapa usingizi ndani ya Jakuzi na Ikh alikuja kukurupuka baadae akakuta mrembo wake kamkubatia vizuri basi alijisikia vizuri sana japo alijua kabisa kesi yake ni nzito sana yaani hadi Naysha aje kumuelewa basi anahitaji kutumia nguvu sana,alianza kulishika tumbo la Naysha ambalo kwa kipindi icho lilikuwa kubwa kabisa alijiskia raha sana kushika tumbo la mkewe huyo kipenzi chake ambaye alifunga naye ndoa ya mchongo,alivochoka aliona kama mwli wa Naysha unapata baridi sana hivyo

aliniynanyua taratibu kabisa akavua manguo yake mabichi akamvua na Naysha taratibu ili asimuamsha maana ilikuwa akilala yaani unaweza mbeba ukaensa kumtupa nje na asijue nasi alimbeba akiwa mtupu akaingia naye chumbani akachagulia Night dress ambalo mara ya mwisho alimnunulia kama zawadi lakin hakumpa akamvalisha akamlaza kitandani taratibu naye akapanda kulala akamkumbatia vizuri mkewe asijr kumponyoka bure.

Asubuhi saa mbili ndo muda ambao Naysha alikurupuka na kukikuta yuko kitandani teba kalala na Ikh mwanaume anayempenda sana basi alijis8kia raha kweli akanyanyuka akashuka chininavowenda kuanza kufanya usafi maana japo alikuwa amechoka sana lakini hakuwa mzembe hata kidogo,nyumba ilkuwa chafu kweli kweli yaani ilikuwa haijafanyia jsafi muda mrefu tu Hivyo alijitahid akafanya usafi taratibu alivomaliza akaenda kuchukua nguo za Ikh akaweka kwenye dry cleaner  alivomaliza akaingia jikoni kwanza akatengeneza supu nzuri na kuweka malimao ya kutosha kwa ajili ya ikh ili atakapoaamka basi aitumie kuondoa Hangover,alivyomaliza alienda

kwenye chumba cha Ikh cha kubadilishia nguo akaweka vitu vyote sawa akampangia nguo vizuri kabisa,alihamia bustanini sasa ambako alikutana na Moze

" Naona sasa mama mjengo umerudi ndo maana leo uja limetoka kusini" aoitania Moze

" We naye hujaachaga tu utani wako jamani" alicheka Naysha maana uyo moze ana matani mabaya kweli

" Lwani uong sasa yaani leo hadi nyumba ina nuru ndani pananukia nukia tu muda wote natamana kujua nini kijapikwa uko aisee"

" Kitu cha kawaida tu bhana Moze sema me nitaondoka so muda apa namalizia tu apa kumwagilia maua alafu nikaoge niondoke"aliovsema ivo Moze alishtuka

" Sasa unaondoka lwenda wapi tena?" aliuliza kwa mshangao

" Si narudi kwetu jaman me apa jana nilikuja tu sababu alinipigia simu akiwa amelewa na siju mkewe yuko wapi hadi anajisumbua mimi" aliongea hivyo Naysha maksudi ili kujua Naiphat yuko wap

" Mkewe yupi kama unamzungumzia Naiphat alishaga timuliwa muda sana hadi tumemsahau si alifanya ujinga na boss hataki hata kumsikia" aliongea moze

" aya bhana ayo mambo yao hayanihusu watajua wenyewe"aliingea Naysha akiwa anaelkea ndani alivofika sebleni alikutana na Ikh

" Hatimaye mlevi umeamka na pombe imeisha kichwan aya supu iyo apo unywe kuondoa  hangover me nataka kurudi kaka ameshanifuata" aliongea Naysha akiwa akiwa anapandisha juu ili kufata handbage yake,Ikh alimdaka mkono

" Mama please naomba tuongee nimechoka sana mwenzio nisamehe mke wangu naomba urudi nyumbani umenikomesha sasa imetosha mama em rudi basi mimi sijakuacha bado" alionga Ikh akiwa amemkubatia Naysba lwa nyuma hadi machozi yalimtoka

" Unaona mama najua nilifanya makosaengi sana kwako lakini sikia we fanya chochote unachotaka niambie chochote me nitafanya nakuoenda Naysha maisha yangu bila wewe naona kabisa hayajakamilika please mama nionee huruma"aliongea Ikh na muda huo Naysha alikuwa kimya kabisa

" Unakumbuka mara ya mwisho uliniambia mimi na  malaya umenifanyia mengi sana ya ajabu unafikiri anwezaje amini kuwa wewe umebadilika na unanipenda ingali mwanzo ulisema huwezi kupenda mwanamke wa aina yangu?" aliuliza Naysha machozi yakiwa yanamtririka maana anaumia kwwli kuwa mbali na mwanajme huyo lakini atafanyaje walati anajua kabisa hapendwi

" Mama upendo huchanua popote na huja wakati ambao hata haukuutarajia na kwangu mimi imekuwa hivyo nilitaka kuishi kwa mazoea lakin yaliniponza miki simpendi Naiphat tena mama kama hofu yako ndo hiyo yule siyo mwanamke wmenye maadili kabisa ukiachana na wazazi hata miki siwezi kabisa kumuoa mama naomba nisamehe naahidi nitafidia makosa na ujinga nilio kufanyia"aliongea Ikh akataman hata apige magoti Ila Naysha akawambia ampe muda afikirie alafu atampa jibu alibeba pochi yake akatoka,Nash alikuwa nje kumsubiri ili waondoke

" Mbona umepoa sana blood shemu kakuboa?" aliuliza hivyo Nash baada ya wao kupanda kwenye gari na kumuona dada yake akiwa kimya na sio kawaida yake

" Blood mimi nashindwa kuelewa nifanye nini nampenda sana Ikh lakin siamini kabisa kama maneno yake anayosema yana ukweli wowote inanichanganya" aliongea Naysha ambaye alionekana kukosa msimamo

" Blood jipe muda wa kufikiria but i think he is so cool sema tu kuna somethings zimacomfuse sana" Nash alimsauri mdog ake ajipe muda maana hatakiwi kukurupuka.

siku hiyo Naysha akiwa hana hili wala lile alipigiwa simu na mama yake mzazi
" Shikamoo mama" alisalima Naysha baada ya kupokea simu
" We mtoto mjaa laana kipi kimekushinda kwenye ndoa yako hadi umeachika hivi huna aibu wewe?" Aliongea mama yake bila hata kupokea salam
" Mama kwani hata nikiachika kuna kitu wewe apo unapungukiwa? mbona kama unaniwakia sana haya ni maisha yangu?"aliongea Naysha maana alishachoka majibu ya mama yake ya ajabu

" Unasemaje wewe ndo maana sijawahi kukuoendavwewe mtot hujuo kama wewe kuachana na Ikh kutasababisha kampuni ya baba yako isambalatike?"
" Hahaa umenichekesha kwani na mimi ni baba yangu jaman hata ikisambalatika me sina hasara yoyote acheni kutumia kivuli changu kufanikisha mambo yenu sasa huyo mwanaume nimeachana naye ni muda wa nyie kupambana na hali zenu" aliongea hivyo Naysha kisha akakata simu maana hakutaka kelele kabisa kwa muda huo kichwa chake hakikuhitaji stress kabisa.

Tukutane swhemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 18 ($2)
Tulipoishia.....
Naysba alikata simu ya mama yake maana alishachoka kuwa dampoo la mama yake yaani kila magumu yakienda upande wake basi lawama zote angepokea yeye na kuambiwa kuwa ni laana zake ndo zinasababisha maisha yake kuwa magumu.

Siku zilisogea Naysha mimba yake ikawa na miezi nane sasa Ikh alijitahid kumbmembelez Sana lakin Naysha alikaza sana alitaka kwanza Ikh aonje dawa yake mwenyewe,hadi mama mkwe alimuomba sana warudiane mwisho akawaambia kama kweli wanashida naye basi wangekuja nyumbani na kufata utaratibu maana mwanzo hawakutoa hata mahali,wakakubali.

Siku hiyo usiku wakiwa kwenye meza ya chakula basi  Naysha ilibid awaambie wazazi wake kuhusu ugeni unatakiwa kuja kesho yake

" Mom and dady kesho tutakuwa na wageni hapa nyumbani Blood i think you know" aliongea hivyo na kumwambia kaka yake kuwa anajua kinachoendelea

" Ugeji gani my twin" aliongea mama wa Nash ambaye alipenda sana kumita Naysha pacha ake kwasababu waliendana tabia karibu kila kitu.

" Twin na baba kesho famikia ya Ikh wanakuja apa nadhani mtawasilikiza" aliongea hivyo na twin wake akafurahi kweli na baba pia alifurahi na kumwambia kuwa anawasubiri kwa hamu sana.

Giza liliazna kuondoka na taratibu kabisa anga likawa jeupe na giza likapisha nuru itawale basi mama Nash aliamka na kuanza kuandaa mazingira akiwa nasaidia na Nash mwenyewe walikuwa na furaha sana yaani utasema sijui ni kitu gani,Naysha yeye kwa muda huo alikuwa kalala tu maana alipaswa kupumzika muda mwingi, Waliweka mazingira sana

Muda ulisogea na ilipofika saa nne kamili basi familia ya Ikh na ikh mwenyewe walifika pale wakapokelewa vizuri tu, sasa Ikh muda sote alikuwa anaaangaza pande zote kujaribu kunangalia kama atamuona Naysha laki hakumuona alikosa raha kweli,hata mama yake Ikh ye alishindwa kuvumilia akauliza

" Toka nimefika hapa sijamuona Naysha yuko wapi?"aliuliza mama Ikh

" Aiii mama unamuulizia blood ni mlalaji hadi basi mimba yake ibampeleka vibaya mno hivyo anaweza lala mpaka hata saa nane,mfano mama hapo alivolala unaweza kumbeba ukaenda kumtupa kwenye dampoo na asiamke" aliongea Nash na kuwafanya wengine wacheke maana aliongeackwa stail yakuchekesha,sasa apo ndo kidog roho ya Ikh ikatulia

" Baba naweza kwenda kumuona?" aliuliza Ikh maana aliona atachelewa kuamka mwisho wa siku waage kuondoka akiwa hajaonana naye

" Nenda tu kijana wangu haina tatizo" aliongea baba wa Naysha,Ikh alinyanyuka na shemeji yake akampeleka hadi malngoni kwa Naysha akamwambia aingie tu ye anarudi seblen

Alivoingia ndani alimkuta Naysha akiwa amelala mwenyewr basi alikaa kitandani akawa anamuangalia jinsi alivyo mrwmbo basi na kimimba kilimpendeza aliinama akabusu tumbo la kipenzi chake mwanamke anayempenda kuliko chochote.

Sebleni basi familia ya Ikh walieleza kilicho waleta na wakaoomba kutoa mahali muda huo huo,kwasababu familia nzima ya mzee Isihaka walikuwa wanajua namna Naysha anavyompenda Ikh basi hawakutaka kumkosesha furaha yake wlikubali mahali ikalipwa basi muda wote Ikh hata hakua ametoka ndani yaani alikuwa anamuangalia mkewe tu na kujilaumu alichelwwa wapi kuuona urembo wa mkewe.

Familia ya Ikh walikaa mpaka jiona kabisa na Naysha alimka akakaa kidogo akasema machoka anataka kulala akarudi kulala tena mpka mudacwa kuondoka Naysha alikuwa kalala basi Ikh aliwaomba ondoke naye Familia nzima walicheka maana Ikh kwacwakati huo hakuonekana kuwa na Subra hata kidogo yaani wakamuuliza utaendaje naye akiwa amelala na hata akimwamusha kuamka basi wangetumia masaa,akwaambia wasijali atambemba hivyo hivyo akiwa kalala akija kuamka atakmjikta akiwa kwake,basi familia nzima walicheka wakiamini kuwa anatania lakin yeye alikuwa serious na muda huo huo wakaona anaburut mabegi akisaidiwa na shemeji yake basi

wazazi wao walicheka na kuambiana kuwa hao mtu na shemeji yake ni kama pipa na mfuniko basi haikuchukua hata dakika kumi basi alitoka akiwa kambemba Naysha akaenda kumwekaa kwenye gari akamuomba baba yake aendeshe ,Nash akamwambia aiswaaumbue wazee atawapeleka yeye.

Saa mbili usiku ndo muda ambao Ikh aliingia sasa rasmi yeye na mkewe aliyekuwa kalala fofofo yaani hajui hata kama kahamishwa mtaa alimshukuru shemeji yake akaingia ndani.

Saa tatu usiku ndo muda ambao Naysha alikurupuka toka usingizini basi aliamka na kujikuta mazingira tofauti alafu kuna kagiza flani hivi akiwa bado anashangaa taa ikawashwa alafu Ikh akasmma

" Supriseeee".

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0687758688

Sehemu: 19  ($2)

Tulipoishia.....

Baada ya Naysha kuamka na kujikuta kwenye mazingira ambayo hata yeye mwenyewe hakuyaelewa basi kabla hajauliza basi Ikh aliwasha taa flani hivi yenye karangi hafifu akasema

" Suprisee" alikngea Ikh akamsogelea Naysha ambye kwanza alikuwa kwenye mshangao

" Nimefikaje uku Ikh wakati nilikuwa nimelala nyumban?" aliuliza Naysha akiwa anakaa vizuri na Ikh akamsaidia kukaa vizuri alafu akamkumbatia

" Nimekuleta mimi apa mke wangu ukiwa umelala mwenyewe hata hukujua kama unaletwa huku pole mwanamke wangu" aliongea Ikh akiwa anambembeleza mkewe

" tabia yako mbaya unawezaje kunibeba nikiwa nimelala kwanini hukusubiri niamke ndo unibbebe?" alikngea Naysha na kukifanya kakasilika

" Nismaehe mke wangu niliona kabisa unachelewa kuamka ndo maana nikakubeba hivyo hivyo" aliongea Ikh

" Bas sogea nikufinye kwanza alafu ndo nikusamehe" aliongea Hivo Naysha akamfanya Ikh acheke

" Me naongea we unajicheka Ikh una dharau?" Naysha alikunja sura Ikh ikabidi abane tu kikcheko chake maana akicheka ataharibu kambi

" Basi sawa mama nismaehe nifinye yaishe" alijongea Ikh akainama ili Naysha mafinye na kweli hamkwepesha alimfinya jap si sana ile finya ya mahaba tu

" mke wangu nikwambie kitu?" alingea Ikh kwa kunong'oneza sikion owa Naysha

" Niambie tu ila kiswe cha kuboa" aliingea Naysha kasauti ka chini

" naomba leo iwe siku yetu ya kufungua ukrasa mpya tusikumbuke ya nyuma mama Nakupenda sana na naahidi kukupend hadi kufa" aliongea Ikh akamkisi mkewe shavun

" Naomba unayoyaonge yawe yakweli kabisa usije kubadilisha kitu" aliongea Naysha basi walianza kupeanan Romance na Ikh akataka mambo lakin Naysha alimwambia hali halisi na akamuomba ikiwezekana basi amvumilis maana docta aliwmambia alsifanye hivyo,uzuri Ikh naye ni muelwa hivyo alimuacha tu akammkumbatia wakala.

Kulivyokucha asubhu  Ikh alimuamsha Naysha mapema ili akafanye mazoezi maana mimba yake ilikuwa inakimbilia miezi tisa hivyo hakutakiwa kuwa mzembe hata kidogo

Naysha alinyanyuka kivivu vivu mumewe akamkokota hadi nje akawa anamfanyisha mazoezi taratibu basi Naysha alikuwa analalamika huyo mara kachoka mara njaa yaani ilikuwa ni usumbufu mtindo mmoja Ikh alikoma basi Moze alivoona wanavohangaishana alicheka hadi basi akajua sasa hapo biss kapatikana.

Zilisikika kelele za madocta wakimwambia mgonjwa " sukuma jitahid" " vuta pumzi sukuma kwa nguvu" nje ya ile wodi ilikuwa ni vituko kuna baadhi ya watu hadi walicheka yaani Ikh na shemji Yake Nash waligeuka wachekeshaj Ghafla maana Ikh alikwa anaenda mbele anarudi mara akae mara anyanyuke anye Nash alikuwa anaenda hadim mlangoni asikilize mara arudi akitoka hap  anaenda kukaa karibu na shemeji yake mara amfute mwenzake jasho basi likuwa ni vituko mwanzo mwisho.Mama Ikh na mama Nash wenyewe walikuwa wamekaa wamtulia kuonyesha wako busy kufanya dua kumuombea Naysha ajifungue salama hata baba zao pia walikuwa na

utulivu kabisa wakiwa wanamuomba Allah Naysha ajifungue salama,baada ya dakika tano basi zilisikika kelele za katoto kachanga kanalia basi Ikh na Shemeji yake yaani waliamka wakawa wanaruka ruka wakaumbatiana kama hawana akili nzuri mmoja akisema anaenda  kuwa mjomba mwingine akisema amekuwa baba kina mama waliokana kushikana mikono ishara ya kupingezana,ambaada ya nusu saa basi waliruhusiwa kuningia kumuona mama na mtoto na doct aliwaambia basi mtot alikuwa ni wakiume familia nzima walifurahi sana.Walivoingi ndani sas Ikh cha kwanza alimuwahi mkewe na Nash akawahi kumuangalia mtoto ety kama anafanana naye basi ilikwa ni vituko tu

sasa nash alivoenda kumuangaliam mtoto akasmea
" God is not fair kwanini huyu kid hajachukua ata sikio langu tu ety kila kitu kamchukua baba yake ni nini hichi" alilalamika Nash kuwa mtoto hajamchukua lwachochote kila kitu ni cha Ikh basi familia nzima walicheka na kumpa pongezi Naysha,ikh alienda kukabeba kaktoto kake basi alijsikiaje raha maana katoto kalimfanan hadi basi yaani hawezi kusema kasingiziwa.

Mtoto aliitiwa Ahan maana ndo nina ambalo baba ake alipendekeza mtot aitwe basi ilishapita mwezi na nusu kina mama walishindana mwanzoni kila mtu alitaka kumtunza Naysha kipindi cha uzazi ikabidi sasa wotevsasa wakutane kwa Ikh ili wamtunze pamoja basi ilikuwa ni vituko maana Naysha alikuwa analishwa vyakula hadi anahis kutapika maana walikuwa kama wanashindana.

Tukutane sehemu ijayo.Simulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard

Whatsapp: 0587758688

Sehemu: 20 ($2)

Tulipoishia.....

Basi baada ya miezi miwili Naysha alikuwa sasa anaweza kujihudumia mwenyewe  mwanae hivyo mama yake na mama mkwe wake waliondoka kurudi makwao.Na kipindi chote hicho basi mama yake hakuwa anfahamau chochote kuhusu yyeye na hakuwa anajua kama Naysha ana mtoto.

Uskku mida ya saa mbili Naysha alikuwa jikon anaandaa chakula mumewe alikuwa yuko na mtoto basi anambadilisha Dippers alivomaliza alikabeba akaenda nacho seblen basi walikuwa wanafurha familia nzima,dakika 20 baadae walikuwa mezani kwaajili ya kupata chakula cha usiku  n Ikh akawa anamlisha mkewe kwasababu kwa muda huo Naysba akikuwa kambeba Ahan anamnyonyesha hivyo iki akawa anamsaidia mkewe kulal

" Kula bha a umhudumuie mwanangu so unakula kama hutaki jaman ndo nin mkevwangu" alilalamika Ikh baada ya mkewe kuwa busy sana na mtoto hadi anasahau kula

" We naye huoni namnyonyesha Ahan me sitaki kusikia makelele yake apa akinyayua mdomo wake na ulivompana basi nakuwa kama napigiwa filimbi maskion" alionge NAYSHA kumkomesha mumewe maana mtoto hakuwa amemfanana yeye hivyo alikuwa namkosoa mtot makusudi kabisa ili baba ake amjibu

" Mke wangu kwahiyo mimi nia mdogo mkubwa embu niangaoie vizuri labda siku hizi macho yako hayaoni vizuri embu niangalie" aliongea Ikh akiwa kamsogezea mkewe uso ety amuangalie vizuri kama kweli ana mdomom mkubwa lbda hakuwahi kumuona vizuri

" Em toka uko bhana unanichelewesha kula mtu hunyamazi jamani" basi ulikuwa ni tani wa hapa na pale kwa wanandoa hao waliokuwa wanapendana na wamepitia misukosuko mingi wakiwa pamoja.

" Alafu nimekumbuk mume wangu kuna kitu naomba unsaifie kama hutojali lakini?" aliongea Naysha kwa upole

" Usijal we sema tu haina tatizo" alijgea Ikh akiwa anachezea vimguu vya mwanae

" Naomba share zako ulizoweka kwenye kampuni ya baba yangu wa kambo uzitoe sihitaji uhusiano wowote na wao nataka kuanza maisha mapya" aliongea kwa upole kweli maana anajua hayo ni mambo ya kibiashara zaidi lakin kwa muda huo hakutaka kabisa kujihususha na mambo ya mama yake wala mume wa mama yake.

" Uaani kabla hata hujaongea mimi nilishafikiria kuhusu hilo yule mzee ni msumbufu sana tu yaani hasaidiki analetwa mambo ya kinyumbani hadi kazini" kumbe Ikh naye tayri alishwaza hivyo sema tu alikuwa anafikiria atamwambia vipi mkewe sasa mke ndo akaanzisha mada hiyo ikabidi ampe mchapo mzima na akawambia wavumilie ndani ya miezi miwili alafu amlipue yule mzee na mkewe wala hata hakubisha.

Ndani ya kampuni ya baba wa Naishia makbo yalionekana kiharibika lwa upande wake hii ni baada tu ya Ikh kutoa hisa zake na kusema hataki uhusiano wowtte wa kibiashara na kampuni yake alihisi kuchanganyikiwa maana hakutegemea kama mambo yangebadilika kiasi hicho maana kwa kipidni chote hicho ambacho Ikh alikuwa amewekeza kwenye kampuni yake basi alikuwa na kiburi kwa kuamin kuwa yuko na mtu mzito hivyo mambo hayawezi kumwendea kombo wanahisa wengi alishawajibu vibaya hivyo alijikut anakosa  msaada hata alipojaribu kuwatafut na kuwaomba msaada,mwisho kabisa tumaini lake lilikuwa kwa watu wawili tu Naishia na

Naysha alipiga simu lwa Naishia kwanza

" Shikamoo baba" alisalimia Naishia

" Marhaba wazima huko?"

" sisi wazima kabisa sijui nyie uko?"

"Sisi tuko salama japo usalam kidogo ni wa mashaka"

" Kun nini?"

" IKH mume wa Naysha ametoa hisa zake kwenye kampuni yetu bila hata sababu ya kueleweka hivyo kampuni ipo kwenye kipindi kigumu sana nahitaji msaada wako mwanangu tofauti na hivyo familia yetu inaenda liwa maskini muda wowote"

" Baba yaani mimi nashindwa hata nikwambiaje mana ninavosema hapa hii familia yenyewe ipo kwenye kipindi kigumu sana mume wangu ameingiza hasara juzi kati hivyo ni ngumu kwa wao kuwapa msaada baba"

Baada y kujibiwa hivyo tumaini lake la mwisho ilikwa ni Naysha alimpigia simu

" Ndiyo mzee nakusikiliza" alionngea Naysha baada ya simu kuwa imepokelewa

" Mwanangu naomba nisaidie ongea na mumeo kampjni yangu inakufa msahwishi arudishe hisa zake tunaenda kuwa maskin" aliongea bana ake Naishia

" Mzee nadhani utakuwa umesahau wewe si ulimuozesha binti yako kwa Bruhan kwa kudai atakuwa msaada utakapo kuwa na matatizo sasa shida nini hadi unajitafuta mimi? sasa ni hivi mimi sina msaada na byie hata familia yako Ikiharibia mimi sina hasara tusitafutane nadhani wa kumtafuta ni mwanao kwaheri" aliongw hivyo Naysha halafu akakt simu maana hakutaka usumbufu kabisa.

Tukutane kwenye sehemu Ijayo.Simulizi: BE WITH YOU
Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 21($2)
Tulipoishia......

Baada ya Naysha kukata simu ya baba yake wa kambo  akawa anaongea mwenyewe

"Mtanisamehe tu kwa hili wewe na familia yako mmeniynanyasa sana bil hata kujali napitia maumivy kiasi gani,ni kuda wenu wa kulipa sasa na kila mtu apambane na hali yake "alijiongelesha Naysha akiwa anaendelea kumnyonyeahha mwanae ambaye kwa muda huo alikuwa na miezi mitano. Na alichukua sura ya baba yake hasswa. Akiwa amekaa alipata ugeni wa ghafla na ugeni huo alikuwa ni Bruhan na mkewe ambaye ni dada wa Naysha,akiwakaribisha ndani

" Karibuni Niwaletee vinywaji gani?" aliongea Naysha kwanza kitu cha kwanza Naishia alishtuka hakutegemea kumkuta hapo mdogo ake maana anavojuaga yeye alishaachwa na Ikh hivyo walikuja apo kwa lengo la kumuomba Ikh msaada maana mambo kwa upande wao yalikuwa mabaya kweli.Sasa wakiwa bado wanashangaa wakasikia sautu ya Ikh toka juu

" Mke wangu Ahan anasumbua bhana me nitamuacha ujue sijui ubishi kachukua kwa nani mtoto bado mdogo" aliongea Ikh na kwa muda huo mtoto wao alikuwa analia Naysha akacheka kwanza

" Italuwa kachukua kiburi chako we unahisi ni cha nani?" Naysha alimjibu akawa anapandisha juu kwenda kumpokea maana katoto kao kalikuwa kabishi hatari,

" Jaman mume wangu yaani unashindwa kumbembeleza mtoto wakati me nilikuwa seblen kuna wageni jaman nenda basi" aliongea Naysha akiwa anambeba mwanae

" Apana twende wote bhana kwan we uku ndani una kazi gani?" Ikh alimwambia mkewe waende wote

Kweli wakaongozana na muda huo Ikh alikuwa kavalia pensi tu na mwanae alikuwa kavaa pens kama yeye

Uku seblen sasa majadiliano yalianza baadaa ya Naysha kutoka
" Ivi Bruhan unawaelewa awa me ninavojua ndoa yao ilikuwa ya mkataba na hawakuwa wanalal pamoja sasa uyo mtoto wamemtoa wapi?" Aliongea Naishia maana hakuweza kuvumilia
" Wewe apa umekuja kuomba msaada au umekuja kucjunguza maisha ya watu we mwanamke mbona uko hivo?" aligomba Bruhan maana aliona sasa kaanza umbea baada ya kufanya kilichomleta hapo.
" Lakini mume wangu nikwambie tue nahisi Naysha amemsingizia Ikh mtoto maana me siamin" hakukoma akaendelea kuongea

" Unafikiri Naysha yuko kama wewe mwenzako anajua nini maana ya uaminifu so kama wewe" Bruhan alimchamba,ndo akaktulia kimya,haukupita muda Ikh na mkewe walikuwa wanakuja yaani toka anashuka hakuw anaaangalia wageni wenyewe ni kina nani alikuwa busy na mtoto wake anamtekenya mpaka Naysha anamkwepesha

" Acha bhana mtoto amecheka sana atapatwa na vichomi jaman muache" aliongea Naysha maana katoto kalikuwa kanacheka atary

" Basi mlete me nimbebe bhana unatunyayasa kama nini mke wangu" alionge Ikh akamchuku mtoto, Naysha akabaki anamuangalia tu  maana alimuita akamwambia mtoto anamsumbua tena saiv kamchukua.Sasa walipofika seblen Naishia jicho lake lote lilikuwa kwa mtoto maana hakutegemea kama hawa wangeluwa pamoja na aliumbuka kweli kweli maana  mtoto alimfanana baba yake hadi alihisi aibu.

" Karibuni jaman aii" yaani Ikh alikuwa anaongea lakin hat hakywatazama uson na mtot alimkwangua akaacha hata kuongea

" Shem sisi tuna haraka  ila tumekuja apa kukuomb msaada utusaidie Kampuni ya mume wangu na baba tumepata changamoto na tumeona tuje kukuomba support yako kidogo" alionge Naishia kwa unyeyekevu alimwambia Ikh shida yao

" Shem kwakweli hilo suala ingefaa umwambie mdogo ako" aliongea Ikh alafu hta akusubiri akambeba mwanae akatoka nje

" Naysha mdogo angu tusaidie wenzio tumekwama em fikiria kuhusu familia yetu" Naishia kwa mara ya kwanza alimuita Naysha mdogo ake

"Sasa Da Naishia me nitakusaudeni nini nilivo sina hata kitu nina msaada gani kwenu nyie?" yaani kwa mateso ambayo alipitia Naysha moyo wa huruma ulishamtoka kabisa

" Mdogo wangu najua sijawahi kukuheshim ata kidogo lakin ni moja ya madhaifu yangu nisamehe mdogo angu em saidia familia ambayo imekukuza"

" ety familia iliyonikuza mbona kama nimeshalipa madeni yote kwenye familia yenu na kuhusu familia mimi hiyo familia hainihusu hata kidogo nina fmilia yangu hivyo tu sina msaada na nyie,Bruham si huyo  na mlisema mkioana mtsaidiana sasa kwanini msisaidiane wenyewe tu" aliongea Naysha maana hakuwa tayari kuwasaidia walijaribu kuongea naye lakini ilishindikana kabisa wakaondoka wakiwa wamelowa.

Ndani y mwezi mmoja tu basi familia ya Bruhan na Naishia zilisambaratika yaani walikuwa weupe tofauti na nyumb hakuna kingine walichomiliki,majuto yote y Bruhan aliyaelekeza kwa Naishia akidai kuwa kama isingekuwa yeye basi familia yake isingesambalatika na muda huo angekuwa na Naysha wake wanaishi vizuri tu na huenda yule mtoto angekuwa wa kwake na Naishia naye alimwambia Bruhan kuwa naye tamaa zakezilimponza.

"Blood  Mshushe jamana amechoka kuruka mwanangu" alionge Naysha wakati huo Kaka yake Nash alikuwa anacheza na mwanae hiyo siku familia nzima walikuwepo yaani yaani kuanzia baba Ikh,mama  Nash,baba Ikh,baba Nash na Nash mwenyewe walikuja kuwatembelea basi ilikuwa furha tu.

" Yaani Naysha na Ikh mjipnge maana uyu mtoto akiacha tu kunyonya namchukua nakaa naye maana nyie watu siwaamini hat kidogo" aliongea Mama Nash

" Weeeee me nilishasema mapema kabisa Ahan nitakaa naye" alidkia mama Ikh yaani hawa wa mama walikuwa wakikaa pamoja ni kushindana tu hawakuwa na kingine zaidi y hicho n walikuwa wanawafanya waume zao wnacheka kweli maana walikuwa kama wanaligi.
" Sasa kwa taarifa yenu mwanangu haend popote atabaki hapa nyumban mke wangu hawezi kukaa mbali nae hata mimi pia" Ikh alimaliza utata kihivo maana hapo wangebishama hadi basi.

Tukutane sehemu ya mwisho panapo majaaliwa ya mwenyezi mungu.

YSimulizi: BE WITH YOU

Mtunzi: Eunice Richard
Whatsapp: 0687758688
Sehemu: 22 final ($2)
Tullipoishia....
Basi familia walikaa pamoj hadi jioni na kila mtu alaenda kwao na Kipindi Icho Nash alishaoa alioa tu mtu mweusi .

Ndani ya mgahawa mmoja walionekana Kwenye mgahawa mmoja Ikh mkewe ambaye kwa kumuangalia tu basi alikuwa na mimba kubwa ty na mtoti wao Ahan ambaye alikuwa na miaka miwili,yaani Ikh hakutaka kuchelewa kabisa akatwanga mimba nyingine na alikuwa anataman ata mkewe asitoke nje kwa kudai ety wanaume wengine watamtamamni na hivyo kma kutoka walikuwa wanatoka pamoja akiwa yuki Off.Sasa muda huo walipoingia pale mgahawani Ikh alikuw kamshika mwanae mkono anatembea Naysha akameambia anataka kwenda chooni mara moja akawaach Ikh na mwanae wakiwa wana oda chakula,sasa akiwa pale alikuja Naiphat akiwa amepauka

kweli na alikuwa mhudumu kwenye ule mgahawa alivomuona Ikh akaanza kulia

" Ikh naomba nisamehe nimejifunza mwenzio ety ndani ya hii miaka nimejua nini maana ya kuheshim upendo wa mtu nakupenda Ikh naomba nisamehe" aliongea Naiphat akiwa analia  maana maisha yalimyoosha

" Me nilishakusamehe muda tu kuwa na aman" aliongea Ikh akwa anamuangalia mwanae ambaye alikuwa anacheza hivyo alikuwa makini kweli asije kuumia

"Unasema kweli Ikh umenisamehe hivyo tunaweza kurudi wote nyumbani,nakuahidi nitakuwa mke mwema kwako" aliongea Naiphat akiamin kuwa amesamehewa na amekubali waturudiane sasa kabla Ikh hajamjibu mwanae alidondoka chini,Ikh alinyanyuka haraka akaebda kumbeba mwanae na muda huo Naysha naye ndo alikuwa anatoka chooni akakuta baba na mtoto wako wanabembelezana

" Nini tena jaman ba Ahan umemdondosha mtoto"aliongea Naysha na kumfanya Naiphat ashtuke yaani hakutegemea kama Ikh angekuwa na Naysha maana aliamn kuwa alishamvurugia hivyo asingeweza kurudi lakini sasa ndo kawakuta pamoja tena wakiwa na mtoto na mimba juu, naysha alivomuona alimwambia tu

" Usitukane mamba kabla hujavuka mto Naiphat pole lakni hilo ni funzo tu kuwa unatakiwa kumuheshim mtu anapokwambia anakupenda" aliongea hivyo Naysha basi Naiphat aliona aibu kweli maana hakutegemwa kabisa aliwahudumia chakula,baada ya kumaliza Naysha alimwambia Ikh ampe Naiphat hela ya mtaji Ikh akatoa laki tano akampa na akamwambia asiwatafute tena.

Usiku Ikh akiwa namkewe ndani wamelala akiwa amemkumbutia mkewe anapapasa tumbo yaani alikuwa anajisikia raha kweli kushika tumbo la mkewe  alikuta anataman at apwwe muda na dunia nzima isimame kwaajili yake awaambie jinsi gani anampenda mkewe  na anajivunia yeye,Basi siku hiyo kuna kitu alikumbuka

" Ivi mke wangu nikuulize kitu" aliuliza Ikh akiwa anaongea taratibu

" ndiyo niulize tu darling" aliongea Naysha kwa mahaba maan hakuwa nyuma

" najua ni swali la kipuuzi na ilifaa aulize mtu wa secondary lakin wacha nikuulize tu,ivi mpaka unaolewa na mimi ulikuwa umelala na wanaume wangapi?" aliuliza Ikh  alafu akavheka maana kweli lilikuwa ni swali la kipuuzi lwa wana ndoa wa miaka mitatu

" Nilishawahi kulala na mwanaume mmoja tu tena nakumbuka niliwekea dawa flani hivi na hata nikiulizwa ni nani nililala naye huwa sikumbuki kabisa na huyo mtu ndo alikuwa wa kwanza kwangu" aliongea Naysha

" Unaweza niambia ilikuwaje maana roho inaniuma uyo alochukua bikra ya mke wangu ni nani?" alionge Ikh kiutani

" Nakumbuka kulikuwa na party ya engagement yaa rafik angu sasa kukbe dasa alituma mtu aje alinyweshe dawa za kunichanganya akili ili tu alale na mimi alafu anaipige picha ili anihaliribie kwa Bruhan maana ndo alikuwa mchumba wangu sasa yeye aliingiwa natamaa na Bruhan mwenyewe alikuwa mshenzi tu maana alikuwa anatwmbea na dada angu kisirisiri"

" Ndo maana siwapendi wale wanadfiki sana enheee ikawaje"

" Sasa ndo alivonipeleka chumbani huyo kaka ndo nikamsikia anavojitapa ye alijua nimezima hivyo baada ya yeye ku8ngia kuoga nilimfungia nikajitahid kutoka na kuingi chumba cha pili ambacho nilikutana na mkaka ambaye alikuwa kalewa kweli ndi akanisaidia akafunga mlango  sasa mimi dawa zilinizidia nikajikuta nimemvamia mkaka w watu na yeye ni mwanaume hakuniacha salama" aliongea Naysha kwa huzuni

" Mbona kama story yako inafanana na yangu kwani ilikuwa hotel gan na chumba" Naysha alitaja hotel hadi chumba ndo Ikh akashtuka na kumwambia kuwa ni yeye aliyelala naye siku zile basi Ikh alijisikia raha kweli kuwa alifungua njia kwa mkewe na akamuoa yeye mwenyewe,basi walicheka.

Mama wa Naysha baada ya kuona mambo yamezidu kuwa mabaya alirudi kwa baba yake Naysha kumuomba msamaha lakin alikuta tayari mwenzake yuko n mkewe wa zamani na wanapendana sana alijaribu kumbembmeleza basi amrudie ata awe mke wa pili lakini Isihaka alimkataa kabisa.Aliamua kumuomba Naysha msamahan akawa anamuomba mtaji Naysha alimpangia nyumba akampa na mtaji lakin hakuchukua hata muda akala mtaji wote,Naysha akaona awe anampelekea hela kidogo na mahutaji yote ya nyumbani ili wasisumbuane.

Naishia yeye kwa upande wake mambo yalizidi kuwa mambaya weupo wote kwisha maana Maisha yalikuwa magumu kweli na wakwe zake hawakuwa wanampenda hata kidog na Bruhan mwenyewe alikuwa mhuni yaani kumbe ilikuwa ni tabia yake na mwisho wa siku wakaishia kukwaaa Ukimwi.

" Mke wangu mwambie mwanangu namsubiri sana aje amuoje kaka yake" aliongea Ikj akiwa anashika tumbo la mkewe wakiwa bafuni wanaoga maji yakiwa yanawatiririkia.

**** *MWISHO*****

Ushauri;

Kwenye maisha bhana watu tunapiti changamoto nyingi sasa unapokutana na matatuzo us8kate tamaa na uwe na imani kuwa kuna kipindi cha furaha kinakuja na angal8a sana huenda watu wako wa karibu ndo wanaokuharibia mambo yako.

Asanteni kwa sapport yenu wadau wangu wa nguvu tukutane kwenye Simulizi inayofuata panapomajaliwa.